# *Mkombozi Wa Jamaa*

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Ni vizuri sana kurudi tena, asubuhi ya leo, kurudi katika nyumba ya Bwana. Ninaamini ilisemwa, wakati mmoja, "Nilifurahi waliponiambia, 'Twende nyumbani kwa Bwana.'"

Charlie, toka nyuma ya nguzo hiyo, uje hapa ukajipatie kiti. Njoo hapa juu. Dada, je, kuna kiti huko nyuma, mahali fulani, tungeweza kujisukumiza? Hapa pana mahali papa hapa *juu*, mama. Njoo papa hapa juu. Hapa, Charlie, njoo hapa uketi karibu na Banks hapa juu, kwa hivyo haitakulazimu kusimama. Kila wakati mvulana huyo anapokuja kutoka huko chini mbali sana Kentucky, akifika hapa, yeye husimama, kila asubuhi. Nasi tutamleta papa hapa juu.

2 Hapa kuna mahali, mwishoni mwa kiti hapa, kwa ajili ya mtu mwingine. [Ndugu Neville anasema, "Kuna mama mmoja hapa nyuma, pia."—Mh.] Kuna mama aliyesimama huko nyuma, nyuma huko. Njoo papa hapa. Hiki hapa kiti papa hapa, dada, karibu kabisa. Songa mbele kabisa. Nami nadhani mtu fulani yuko kwenye kiti cha magurudumu pale. Sivyo? [Dada mmoja anasema, "Ndugu Branham?"] Naam. ["Kuna kiti papa hapa."] Kuna kiti kingine papa *hapa*. Ikiwa mtu anataka kimoja, nyuma huko nyuma, papa *hapa* pana kiti papa hapa. [Ndugu fulani anasema, "Na hapa kuna kimoja, Ndugu Branham."] Hiki hapa kimoja papa hapa juu, pia, jistareheshe. ["Kingine, hapa."] Naam. Unaweza kupata kimoja papa hapa. Sasa, njoni huku, ketini. Na mjisikie ninii hasa . . .

3 Tunataka mstarehe wakati tukijaribu kuleta Neno la Bwana. Loo, bila shaka ni vema kuwa hapa.

4 Sijamwona Charlie jukwaani. Je, yuko huko nyuma? Vema, mleteni hapa. Jamani! Nimekuwa na Charlie, kule chini, siku chache zilizopita, wala siwezi kupita bila kwenda nyumbani kwake na kula, kwa hivyo nitamleta jukwaani, asubuhi ya leo. Kila siku akija hapa, husimama karibu na ukuta pale, kumpa mtu kiti. Kwa hivyo niliangalia huko nje asubuhi ya leo na kumwona amesimama pale, nikawazia, "Nita—Nitamleta humu ndani sasa." Vema, ni—ni sawa. Sasa tutapata ujumbe asubuhi ya leo kutoka kwa Ndugu Russell Cox. [Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka—Mh.] Nellie yuko wapi? Mimi . . . Hiyo itakuwa safari nzuri kwake. Wapi? Naam. Jambo ndilo hilo.

5 Vema, hakika nina furaha kuona wengi wa marafiki huku. Jumapili iliyopita nilipoondoka, nilijisikia vibaya wiki nzima. Nilikuwa na rafiki mzuri aliyeketi hapa, kutoka huko chini kabisa Kusini, Ndugu West. Na nilikuwa nimezunguka, kupitia kwenye kusanyiko, nimechelewa. Nikasema, "Nina furaha

kumwona *Fulani* na *Fulani*," nami nikamruka Ndugu West, wala kamwe—kamwe sikumtambua hata alipoanza kutoka nje. Ndipo nikawazia, wiki nzima, "Ndugu West atadhani si—sikumjali makusudi." Lakini yeye ni—yeye ni Mkristo, kwa hivyo anajua bora kuliko hayo. Anajua kuwa mimi . . . rafiki wa kweli. Nami najua anajua, nisingefanya hivyo.

6 Nilikuwa nikifikiria asubuhi ya leo, nikishuka kuja, kuwaona watu ambao wametoka sehemu mbalimbali. Sasa, huyu hapa Ndugu West hapa tena, asubuhi ya leo. Na Ndugu na Dada Kidd hapa, kutoka Ohio. Na baadhi ya ninii wangu . . .

Najua Ndugu Evans yuko hapa. Nilienda kumwona, jana alasiri, kwenye moteli, lakini nadhani alikuwa ametoka pamoja na Ndugu Fred na hao wengine. Nao wanakuja kutoka huko mbali Macon, Georgia, hapa, kila Jumapili ninapohubiri. Kutoka Macon, Georgia, hiyo ni mbali sana huko chini. Ni kama maili mia nane, au zaidi, nadhani, huko chini. Kuendesha gari pamoja na familia yake, kila siku ninapohubiri. Na huo ni uaminifu.

7 Nami nilikuwa—nilikuwa nikiwazia, loo, basi, kama una marafiki kama hao, wanaotaka kusimama na wewe! Sasa, hiyo . . . hao watu hawatoki huko mbali Georgia, na Ohio, na sehemu mbalimbali za taifa, kuja kwenye maskani hii ndogo hapa, kunisikia mimi. Wanakuja hapa kwa sababu wanaamini Ujumbe huo. Huo ndio wanaoamini. Wanaamini Ujumbe huo. Basi ninapaswa kuwa mwaminifu na mkweli juu ya Ujumbe huo jinsi gani! Kwa sababu, sio—sio tu kwamba mimi, ninakosea, lakini ninamwongoza mtu mwingine vibaya. Mnaona? Ndipo basi Mungu ataniwajibisha kwa kosa lao, kwa sababu mimi ndiye niliyefundisha hilo. Mnaona?

8 Nami nawaambia, hakika inakufanya ufikirie kindani unapowazia mambo kama hayo. Kwa hivyo na—nathamini kila mmoja wenu, ni vizuri sana kujua kwamba ungeendesha gari hayo mamia ya maili, kupitia barabara zenye hatari na juu ya barabara hizi kuu, ambapo ajali na kadhalika. Imani yenu katika Mungu huwaongoza, kwa namna fulani, inawaleta hapa na kuwarudisha. Tuna furaha sana kuwa na marafiki wa aina hiyo. Ninaomba baraka nyingi za Mungu juu yenu.

9 Sasa, Jumapili iliyopita, ni—nilisema, "Vema, tutazungumza, kisha nitaitisha tu mstari wa maombi." Nimekuwa nikijaribu kutafuta njia fulani, kujaribu kupata njia ya kuwaombea watu wengi zaidi. Na kama nikiwapitisha wengi zaidi kama Jumapili iliyopita, mimi . . . mtu fulani atakuwa akiniombea. Niliondoka hapa, karibu saa nane. Wala si—sikusambaza kadi za maombi.

10 Kusambaza kadi za maombi ni kazi ngumu. Sijui kama mnajua hivyo, au la, watu wanakuchukia. Naye Ndugu Banks Wood, alisema, hivi majuzi, tulipokuwa huko Kentucky,

kwamba angejitolea na kusambaza kadi za maombi ikiwa Billy hakuingia. Kwa hivyo Billy, kwa kuwa ni mwanangu, mwajua, mbona, wao . . . Mimi hupata barua chache, "Aliniahidi kadi ya maombi na hakunipa. Maskini mtundu huyo!" Kwa hivyo wao . . . Hawezi kuzisambazia kila mtu. Wala hatuwezi kuwaweka wengi kupita kiasi mstarini! Mnaona? Hana budi kunilinda.

11 Basi—basi tulipotoka, binti-mkwe wangu alisema, "Bill, itabidi umrudishe Billy huko nyuma na kadi za maombi, au," kasema, "hutadumu sana."

12 Na, kwa hivyo, lakini ambapo nilifanyia kosa, ilikuwa ni kuanza utambuzi, kisha mtu fulani akarudi, kasema, "Nilisahau, mama alitaka kuombewa." Mnajua sababu ya kurudi kwao, ni kwa ajili ya utambuzi huo, mnaona. Kwa hivyo, lakini, siwalaumu. Ningefanya jambo lile lile. Mnaona? Ningefanya ninii . . . Sisi ni wanadamu, na sisi sote tunataka kuishi, na tunataka kujua la kufanya. Ndivyo tulivyo . . . Lakini unaweza tu kwenda umbali huo na mambo hayo, wewe, ya karama, ndipo basi karibu umekwisha, wakati mara kadhaa hilo linapotukia.

13 Na kwa hivyo Ndugu Banks alikuwa asambaze kadi za maombi asubuhi ya leo, ndipo ikatokea kwamba Billy aliingia jana usiku. Kwa hivyo nilifikiri hilo lingekuwa baya sana, kumwacha mtu mwenye sifa nzuri, mambo kama Ndugu Wood, kuzisambaza kadi za maombi, kufanya watu wamwingilie. Nadhani Billy hajali. Amekuwa na hayo muda mrefu sana, kwa hivyo yeye huyaachilia tu. Vema.

14 Sasa—sasa wiki hii ijayo ninapaswa kuwa Dallas, Ijumaa hii ijayo usiku, kwenye mkutano wa Sauti ya Uponyaji. Ikiwa kuna watu wowote karibu na hapo, ninapaswa kuwa huko usiku huo mmoja, kuzungumza katika mkutano wao. Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la *Njia ya Kuuendea Ushirika*, Bwana akipenda.

15 Na halafu, labda, labda Jumapili inayofuata, hiyo itakuwa Jumapili hii ijayo, Bwana akipenda. Sasa sina hakika sana. Bwana akipenda, ninataka kurudi na kuzungumza juu ya somo ambalo nilipaswa kuzungumzia leo hii, *Upepo Katika Kimbunga*. Nami nilikuwa niwaombee wagonjwa, leo. Na hiyo kwa namna fulani ni kemeo kali kwa—kwa kanisa kwa ajili ya dhambi zake. Na—na hilo si somo zuri sana kuzungumzia wakati unapoenda kuitisha mstari wa maombi. Unapaswa kujenga imani ya watu kwa . . . kwa maombi, na kwa Mungu, na kuwa na imani. Kwa hivyo nilimwambia Ndugu Neville atangaze kwamba nitazungumza asubuhi hii juu ya somo lingine, kujenga imani katika watu, kwa Mungu. Kwa maneno mengine, kuwakemea watu kwa—kwa kutozishika amri za Mungu. Kwa njia hii, inawajenga watu huku, kuwa na imani katika Mungu. Mnaona?

16 Na nyuma katika chumba cha maombi asubuhi ya leo, au chumba cha kurekodia kule nyuma, maskini rafiki yangu wa zamani, Ndugu Kidd, themanini na, umri wa miaka themanini, anayeketi hapa. Wengi wenu mnakumbuka nilipomkimbilia hivi majuzi asubuhi, alikuwa—alikuwa karibu. . . imekuwa karibu mwaka mmoja uliopita, karibu nao sasa. Akifa, mahututi sana, nao madaktari wakampa wiki moja ya kuishi. Au, sio wiki, wao. . . Asingeweza kuishi kufikia asubuhi apate kuletwa huku chini, karibu asubuhi tatu zilizopita. Na sasa alikuwa ameshuka hadi mia moja na tano, au kitu kama hicho. Alisema, dakika chache zilizopita, amerudi kwenye mia na thelathini na mbili. Alisema alijisikia kama mvulana.

17 Ndugu Kidd, nashangaa ikiwa ungeweza kusimama tu, watu wapate kujua mhubiri huyu mzee ni nani. Huyo hapo. Hebu tuseme, "Asante Bwana." [Kusanyiko linasema, "Asante Bwana!"—Mh.] Mtu akifa kwa kansa, katika hiyo—katika hali hiyo. Anaye maskini mwenziwe mzuri hapo. Laiti angalisimama, pia. Ninaninii tu. . . Dada Kidd, vipi kuhusu wewe kusimama hapo? Sasa, yeye. . . Mnaona jinsi anavyoweza kuamka haraka? Haraka kuliko ninavyoweza. Mungu awabariki Ndugu na Dada Kidd. Baraka nyingi za Mungu na ziwe juu . . . Asante, dada.

18 Wanajitahidi kupitia milima ya Kentucky, juu chini kwenye njia za eneo la makaa ya mawe, wanafukuzwa, wanatupwa nje, na kudhihakiwa, wanateswa, wanaishi kwa chochote wawezacho. Wanasaga mahindi ambayo wangeyapata njiani, mahali fulani, na kuuishia Ufalme wa Mungu. Na umri wa miaka themanini, wakihubiri Injili, bado. Sasa, wamezeeka sana hawawezi kutoka nje, kwa hivyo mimi huombea vitambaa vya maombi na kuwatumia, na wao wa—wanaendelea tu kuvipeleka hospitalini na vitu kama hivyo. Watu huja na kuvichukua. Sasa, huko kweli ni kuwa nalo moyoni. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ikiwa huwezi kwenda huko nje kukutana nao, unaweza kuwatumia kitambaa cha maombi, namna hiyo, watu wakiwa na imani. Hilo ni zuri sana.

19 Ndugu Rogers ameingia, pia, mahali fulani humu ndani leo, baba mkwe wa Ndugu Creech, rafiki yangu mpendwa sana. Huenda nyumbani kwake kama vile tu ninavyoshuka kwenda kwa Charlie na kwa Nellie na huko chini sasa, na kule Kentucky. Basi—basi nilikuwa nikienda kule chini na kuwinda, wakati wote, pamoja naye. Na hapa, si muda mrefu uliopita, yapata miezi kumi na mitatu iliyopita, daktari alimfanyia upasuaji. "Akiwa na kansa, na," akasema, "amekwisha."

20 Ndipo nikawazia, "Maskini rafiki yangu wa thamani!" Askari mkongwe, Vita vya Kwanza vya Dunia, mtu shujaa kweli, familia yake. Nami nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, miaka mingi iliyopita, kwa ondoleo la dhambi yake, nikijua basi kwamba aliwekwa katika Mwili wa Kristo, naye alikuwa tayari kwenda kumlaki Mungu. Nikawazia, "Ndugu yangu wa thamani

atatuacha sasa." Ilikuwa mara tu baada ya ono lile, au kabla ya ono hilo kunijia, kuhusu Mbinguni. Basi nikashuka kwenda kumwona, ndipo humo chumbani ukaja upinde wa mvua. Mungu akayabadilisha mambo. Hiyo imekuwa miezi kumi na mitatu iliyopita, na bado yuko hapa leo, akila.

21 Alimeza aina fulani, akameza aina fulani ya vidonge vya salfa, vikamchoma kooni mwake *hapa*. Naye atakuwa katika mstari wa maombi, nadhani, asubuhi ya leo, ujao. Nami najua kwamba ninatangaza hilo Billy akiisha kuzisambaza, au akienda kuzisambaza, walijua ya kwamba watasambaza kadi za maombi. Nilimwambia mkwewe, rafiki yangu mwema, Ndugu Creech, amlete—amlete huku. Ndipo nikawazia, kama nikimkosa, basi nitamkamata na kumweka katika moja ya vyumba hivi vya maombi hapa. Lakini alikuwa na kadi ya maombi. Nami nikasema, "Busty, nataka uende huko nje." Jina lake ni Everett. Tunamwita tu Busty, kwa kifupi. Na yeye—yeye. . . Nikamwambia, "Toka uende kwenye mstari wa maombi. Afadhali nikuombee wakati upako upo, kwa ajili ya huo." Kwa hivyo napenda kuwa na. . . Ikiwa najua nilikuwa nikiombewa, ninataka mtu awe na upako wakati wakiniombea.

22 Sasa hebu tufungue katika Biblia yetu, asubuhi ya leo, tufungue Kitabu cha Ruthu. Nitasoma Maandiko kutoka kwenye hiki, kutoka kwenye Kitabu cha Ruthu. Na sasa kabla tu hatujakaribia somo hili. . . Nikiweza, ningependa kutangaza somo langu la asubuhi ya leo, linaitwa: *Mkombozi Wa Jamaa*. Nami ningetaka kuliendea kutoka kwa misimamo minne mbalimbali, juu ya ukombozi.

23 Nikiwazia, Jumapili iliyopita, nilikuwa nikihubiri juu ya jinsi Kristo alivyokuja kutukomboa. Halafu basi, leo, ninataka kuzungumza juu ya: Mkombozi ni nini? Anakuwaje Mkombozi? Basi, kumbukeni, Mkombozi anakukomboa kabisa, wakati Yeye anapokukomboa; kutoka kwa dhambi zako, kutoka kwa ugonjwa wako, kutoka kwa kila kitu ambacho sio sawa. Yeye ni Mkombozi.

24 Sasa, kabla hatujalikaribia, hebu tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza na Yeye, kwa maombi. Na sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, sijui ni wangapi asubuhi ya leo, katika Uwepo, wangependa kukumbukwa katika maombi, kwa kuinua mikono yenu na kusema, "Mungu, unaona. . . unajua haja yangu"? Mungu awabariki, kila mmoja.

25 Baba yetu wa Mbinguni, nina furaha sana, leo, kwamba kuna Nguvu kubwa za Juu, tukijua kwamba, Mungu, kwamba tunaweza kukaribia kupitia Mwanawe, Kristo Yesu, na kupata ji—jibu kwa kile tunachoomba. Kama vile katika mkutano uliopita, tulikuwa tukiongea juu ya jinsi watu walivyotangatanga huku wamevaa ngozi ya kondoo na ngozi za mbuzi, na walikuwa ukiwa, wakitafuta Mji ambao

mwenye kuubuni na kuujenga alikuwa Mungu. Wakijua laiti wangaliweza kamwe kumwendea mara moja, laiti wangeweza kupata mahali alipokuwa! Kama Ayubu, wa kale, alivyosema, "Laiti ningeweza kwenda, niubishe mlango Wake," kwa maneno mengine. "Laiti ningeweza kupata mahali Yeye—Yeye anapokaa, ningeenda Nyumbani pamoja Naye, na ninge—ningeongea Naye, ana kwa ana." Lakini hakukuwako na njia ya mwanadamu kufanya hivyo, kwa sababu alikuwa ametenda dhambi, naye alikuwa amejitenga akawa mgeni kwa Mungu.

26 Lakini kupitia Yule wa thamani Ambaye alikuja na kufungua njia, na kusamehe dhambi zetu, na kutuleta mbele za Mungu, si kama wageni, bali kama watoto wanaomwendea Baba yao. Tukijua kuwa atatujalia kila haja tunayoomba. Sheria moja tu imewekwa, ambayo ni, "Kama unaweza kuamini." Hayo ndiyo mapatano. Shetani anadai kwamba hatutaamini, naye Mungu anasema tutaamini. Sasa vita vimepamba moto, na uamuzi ni wetu kufanya. Vyovyote uamuzi wetu utakavyofanywa, hivyo ndivyo itakavyokuwa. Na imeandikwa vizuri sana, "Mambo yote yanawezekana kwa hao wanaoamini."

27 Nasi tunaamini, leo, tunakuja, tukikukaribia Wewe tupate kibali cha Kiungu, tukiomba kwamba Wewe utayazingatia maombi yetu. Na kila mkono ulioinuliwa, Wewe unajua chini ya mkono huo, moyoni mwao, yaliyomaanishwa. Kwa maana imeandikwa, kwamba, "Wewe unajua makusudi na mawazo ya nia, na unaweza kuitambua nia." Nasi tunaomba, Mungu, kwamba utajibu kulingana na utajiri Wako na neema Yako, kila haja ambayo ilitajwa.

28 Tungeomba pia leo, Bwana, kwamba utanisaidia, anayehitajika zaidi, labda, wa hili kusanyiko; nikijua kwamba, waliowekwa mbele zangu hapa, ni wale walionunuliwa kwa Damu ya Bwana Yesu. Kunao, labda, wenye dhambi wanaoketi hapa, ambao wamefungwa sana na dhambi, hata ingekuwa ni vigumu kwao, karibu haiwezekani, kwao kufikia mahali pa kumpokea Kristo, maadamu Shetani amewafunga kwa nguvu zake. Lakini tukijua ya kuwa imeandikwa, "Katika Jina Langu watatoa pepo."

29 Na utupe nguvu leo, Bwana, kupitia mahubiri ya Neno, kumtoa kila pepo wa shaka na ushirikina na hofu, kutoka kwa mioyo na akili za watu. Ili wale ambao wamefungwa na vurugu na mashaka wapate kuletwa mikononi mwa Kristo. Na pia imeandikwa, kwamba, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya." Kuna wale hapa ambao ni Wakristo, nao wamefungwa na pepo wa magonjwa.

30 Bwana, nipe nguvu leo, za Roho Mtakatifu, kumkomboa kila mgonjwa na anayeteseka aliye humu jengoni leo, ili Roho Mtakatifu mkuu apate kuwa na ukuu katika kila moyo na kila mtu aliye katika Uwepo wa Kiungu.

Nena nasi kupitia Neno Lako. Neno Lako ni Kweli. Bila kujua la kusema, lakini nikingojea uongozi wa Roho Mtakatifu, ili aweze kutuongoza na kutuelekeza katika Kweli yote. Lijalie, Bwana. Jipatie Mwenyewe utukufu. Na umtie mafuta mtumishi Wako. Nalo Neno Lako tayari limepakwa mafuta. Tutakupa sifa, wakati ukilipeleka kwenye kila moyo, kama tulivyo na haja. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba, Mwana wa Mungu. Amina.

31 Kabla ya kusoma, huenda nikasema msemo huu mdogo niupendao sana:

> Ikiwa una mito usiyoweza kuvuka,
> Na una milima usiyoweza kupitia,
> Kumbuka tu, Mungu Mbinguni ni mtaalamu
> katika mambo wasiyoweza kufanya wengine.

32 Ninasoma kutoka Kitabu cha Ruthu, mlango wa kwanza.

> *Ikawa zamani za Waamuzi walipoamua, kulikuwa na njaa katika nchi. Akaondoka mtu mmoja wa Beth-lehemu ya Yuda, akaenda kukaa katika nchi ya Moabu, yeye, na mkewe, na wanawe wawili.*
>
> *Na jina la mtu huyo aliitwa Elimeleki, na . . . mkewe Naomi, . . . jina la . . . wanawe Maloni na Kilioni, Waefrathi wa Beth-lehemu ya Yuda. Wakafika katika nchi ya Moabu, wakakaa huko.*
>
> *Akafa Elimeleki, mumewe Naomi; . . . yule mwanamke akasalia, na wanawe wawili.*
>
> *Nao wakaoa wake katika wanawake wa Moabu; na jina la . . . mmoja aliitwa Orpa, . . . jina la wa pili Ruthu:* wakakaa *huko yapata miaka kumi.*
>
> *. . . Wakafa na Maloni na Kilioni wote wawili; na hao wanawake wakafiwa . . . huyo mwanamke akawa amefiwa na wanawe wawili, na mumewe pia.*
>
> Ndipo *alipoondoka, yeye na* mkwewe*, ili kurudi kutoka nchi ya Moabu: maana yeye . . . amesikia katika . . .* amesikia *ya kwamba BWANA* amewajilia *watu wake na kuwapa chakula.*
>
> *Basi akatoka pale alipokuwapo, na* wakweze *wawili pamoja naye; wakashika njia ili warudi mpaka nchi ya Yuda.*
>
> *Kisha Naomi akawaambia* wakweze *wawili, Nendeni sasa mkarejee kila mmoja nyumbani kwa mamaye: BWANA na awatendee mema nanyi, kama ninyi mlivyowatendea mema hao waliofariki na mimi pia.*
>
> *BWANA* na *awajalie kuona raha kila mmoja nyumbani kwa mumewe. Kisha akawabusu; nao wakapaza* sauti *zao wakalia.*

*Wakamwambia, La, sivyo, lakini tutarudi pamoja nawe kwa watu wako.*

*Naye Naomi akasema, Enyi wanangu, mrejee: kwa nini* ninyi *kufuatana na mimi? Je, mimi ninao watoto wa kiume tena tumboni mwangu, hata mweze . . . hata . . . wawe* mume *wenu?*

*Enyi wanangu, mrejee, nendeni zenu; kwa kuwa mimi ni mzee siwezi kupata mume tena. Kama ningesema, Natumaini, kama ningempata mume hata usiku huu, na kuzaa watoto wa kiume;*

*Je, mngesubiri* hata *watakapokuwa watu wazima? Mngewangojea . . .* kwa ajili yao *. . . mngejizuia msiwe na waume? La, sivyo, wanangu; maana ninaona uchungu sana kwa* ajili *yenu, kwa sababu mkono wa* B*WANA* *umetoka juu yangu.*

*Nao wakapaza* sauti *zao, wakalia tena: na Orpa akambusu mkwewe; lakini Ruthu akaambatana naye.*

*Akasema, Tazama, shemeji yako amerudi kwa watu wake, na kwa* mungu *wake: basi urejee wewe umfuate shemeji yako.*

*Naye Ruthu akasema, Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe: maana wewe* uendako *nitakwenda; na wewe ukaapo, nitakaa: watu wako watakuwa watu wangu, . . . Mungu wako atakuwa Mungu wangu:*

*Pale utakapokufa, nitakufa nami, na papo hapo nitazikwa:* B*WANA* *anitendee hivyo na kuzidi, ila kufa tu kutatutenga* mimi na *. . . wewe nami.*

33 Ninataka kuyaita mazungumzo haya madogo asubuhi ya leo, ninapoyafundisha, nikijaribu kuleta imani kwenu, ya ukombozi, na kwamba ni nini, na jinsi ya kuupokea. Nataka kuyaita: *Mkombozi Wa Jamaa.*

34 Sasa, *kukomboa* chochote, ni "kukirudisha." Kitu ambacho kimepotea, kama vile kuweka kwenye duka la rehani. Nawe unashuka na kukikomboa hicho, kinakombolewa kwa gharama. Ndipo ni mali yako ya kibinafsi, ukiisha kukikomboa. Lakini sheria ya ukombozi, katika Israeli, ilibidi iwe ni mtu wa jamaa, kuikomboa mali ama kitu kilichokuwa kimepotea.

35 Hadithi yetu inaanza wakati wa watawala wa Israeli, ambao walikuwa ni waamuzi, baada ya kifo cha Yoshua. Na kupata picha nzuri sana ya hii, soma yapata milango ya kwanza mitano au sita ya Samweli wa Kwanza, nawe uta—utapata hadithi yake halisi.

36 Lakini tutaruka sasa kupata muktadha mkuu kutoka kwa hili. Ambayo, wakati fulani uliopita, nilianza kwenye Kitabu hiki cha Ruthu, nami ilinichukua wiki tatu au nne, nikikipitia. Nilianza kwenye Kitabu cha Ufunuo, siku moja, na ikanichukua

mwaka mzima, karibu hivyo, kukipitia. Kila Andiko dogo linaungana moja kwa moja na lingine, kabisa, kote katika Biblia. Inapendeza. Kwa hivyo, tunajua Biblia imevuviwa. Kwa maana, kihisabati na kila njia, hakuna kitabu kingine kilichoandikwa ambacho hakitajipinga mahali fulani.

37 Kitabu hiki kiliandikwa kwa kipindi cha karibu miaka elfu nne, Vitabu vya Biblia. Navyo viliandikwa na baadhi... Ninasahau ni watu wangapi walioviandika. Nilikumbuka. Lakini, samahani. Ninataka kusema sitini na kitu, lakini mimi—mimi ni—mimi ni...Huenda nikakosea hapo. [Ndugu mmoja anasema, "Arobaini."—Mh.] Arobaini. Watu arobaini waliiandika Biblia, katika kipindi cha maelfu ya miaka, bila kujuana, wala kuonana, au kusoma baada ya mwingine, mara nyingi. Wala hakuna neno moja linalolipinga lingine. Imevuviwa!

38 Sasa, watu wengi wanaangalia Kitabu hiki cha Ruthu, kama wasemavyo, "Ni hadithi ya mapenzi ya Biblia." Biblia ni hadithi ya mapenzi. Biblia nzima ni hadithi ya mapenzi.

39 Sio tu kwamba ni hadithi ya mapenzi, bali ni nabii. Sio kwamba tu ni nabii, lakini pia ni historia. Sio kwamba tu ni ha—hadithi ya mapenzi, historia, nabii, ni Mungu Mwenyewe. Kwa sababu, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Kwa hivyo, Neno ni Mungu katika maandishi. Hilo linapaswa kulitatua, ndugu; Mungu katika maandishi. Yehova, akichapishwa kwenye Kitabu. Na hakuna moja yake iliyo namna fulani tu ya hadithi ya uwongo, lakini yote ni Ukweli mtupu. Kila sehemu Yake, iweke nafsi yako. Iko Hapo. Ni Ukweli, na Mungu atalitetea Neno Lake.

40 Nayo hadithi hii iliandikwa, na hati zote za kale. Wakati walipokuwa wakiitenganisha Biblia, wale watu watakatifu, wakati walipokuwa wakijaribu kuiweka pamoja katika Agano la Kale, Kitabu hiki cha Ruthu kilikuwa kimoja cha Vitabu bora sana ambavyo walivikubali. Kwa nini? Ikiwa ni hadithi tu ya mapenzi, kwa nini waandishi na wahenga wa kale wakubali Kitabu hiki kuwa kimevuviwa? Kwa sababu, kuna ufunuo uliofichwa ndani Yake. Na katika ufunuo huu uliofichwa, unapata maana halisi. Utakuleta karibu sana na Mungu.

41 Nami naomba, nafsi yangu yote, asubuhi ya leo, kwamba Mungu ataushika kila moyo, auduwaze kabisa, hata ajifunue Mwenyewe, kile tu alicho, katika hadithi hii; kile Yeye alicho kwako; jinsi ya kumkubali. Na mara ukiliona, ni rahisi sana, unashangaa jinsi gani ulivyopata kupita juu yake. Lakini inaweza kufunuliwa tu na Roho Mtakatifu.

42 Sasa, wengi, wanapoisoma Biblia, wanaisoma, wanasimama tu na kusoma ukurasa, na kusoma ukurasa. Hutaipata kamwe. Kwa sababu, iko katika vitendawili. Naye Yesu alimshukuru

Mungu kwa kuifanya hivyo. Kasema, "Umeificha kutoka kwa macho ya wenye busara na wenye akili, na utaifunua kwa watoto watakaojifunza."

43 Kama vile nimesema mara nyingi. Bibi Branham aliyeketi pale nyuma, asubuhi ya leo. Lakini nikiwa nchi za ng'ambo, ataniandikia barua. Atasema, "Mpendwa Bill, nimeketi hapa, usiku wa leo, pamoja na watoto. Ninakuwazia." Ndipo anaendelea na kuandika kile atakachoandika. Lakini na—nampenda, na ninamjua vizuri sana, naweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua haswa anachosema, unaona, ikiwa atayaandika hapa au la. Mnaona? Maana, najua anachosema. Kwa nini hivyo? Hayo ni mawasiliano ya karibu. Sisi ni mmoja. Unaona? Naye anajua tabia yangu, najua yake. Yeye hana . . .

44 Anaweza tu kuketi na kuniangalia. Ninaweza kukwambia anayoenda kusema, unaona, kwa sababu na—namjua vizuri hivyo. Naye anaweza kunifanya vile vile. Sasa, ni nini kinachofanya hivyo, ni kuaminiana. Upendo!

45 Jana asubuhi, tulikuwa tumelala kitandani tumechelewa kidogo, na watoto hawakulazimika kwenda shuleni, basi tukaanza kuzungumza juu ya mambo mbalimbali. Na jinsi . . . "Chuki ilikuwa nini?"

46 Nilisema, "Chuki ilikuwa na mwanzo, kwa hivyo haina budi kuwa na mwisho. Upendo haukuwa na mwanzo, kwa hivyo hauna mwisho. Chuki ni ya enzi na enzi. Upendo ni wa Milele. Chuki huanza na chuki itaisha. Upendo haukuanza kamwe na hautaisha kamwe." Unaona? Ulikuwa wa Milele.

47 Basi mwanamume anapompenda mwanamke na kumuoa kwa sababu ni mrembo tu, huo utakuwa na mwisho. Lakini mtu anapompata mwanamke ambaye anampenda, hajui ni kwa nini, lakini anampenda. Naye anampata mwanamume ambaye anampenda, bila kujali sura yake. Mwanamume anampenda mwanamke. Mwanamke anampenda. Huyo ni mwenzi wa Milele katika Utukufu. Wata- . . . Mauti wala kitu kingine chochote hakiwezi kuwatenganisha, kwa sababu wametoka Umilele. Ndipo wakatoka nje, katika kipindi cha wakati, nao watarudi katika Umilele. Umilele umeshuka chini katika mwili, unaoitwa wakati, kisha unarudi tena katika Umilele. Hauwezi kuangamia.

48 Mwanamke ambaye ni mrembo, urembo huo utafifia, hakika tu. Hebu upe miaka michache. Labda, leo, anajinyonganyonga mtaani, maskini mwanamke fulani nusu uchi, akizipeleka nafsi nyingi kuzimu kuliko vyumba vyote vya pombe nchini. Lakini atajinyonganyonga mtaani, akifikiria yeye ni kitu. Kama vile Biblia ilivyosema, "Wangekuwa na shingo zilizonyoshwa, kutamanisha, *hatua za madaha*," (hiyo inamaanisha kujinyonganyonga) "wanapotembea," katika siku za mwisho. Wakitimiza Maandiko, wala hawajui. Wanasimama

uani, wamevaa nguo zinifu, wanaume wakimwangalia, wala hajui. Anaweza kuwa mwadilifu sana, kwa mumewe au mpenzi wake mvulana, kadri awezavyo kuwa; lakini, kwenye Siku ya Hukumu, atawajibika kwa kuzini na mamia ya wanaume. Roho juu yao, wala hawajui. Biblia ilisema, "Uchi, kipofu, wala hujui." Sehemu ya kusikitisha ni, "Hujui."

49 Lakini je, ulijua, maskini umbo hilo lililoumbika, ambalo Mungu amempa msichana huyo, huenda likawa limeoza kwenye wakati huu Jumapili ijayo? Mtu huyo mrefu, mweusi na mwenye sura nzuri anaweza kuwa si kitu ila tu lundo la takataka, kufikia Jumapili ijayo. Hiyo yote huangamia.

Lakini kile kilicho ndani, Mungu, upendo, huishi Milele. Kwa hivyo, angalia ndani. Elekeza macho yako kwenye lengo.

50 Sasa, hadithi hii inaanzisha kitu cha namna hiyo, kama mwanamke anayependeka, mzuri. Jina lake aliitwa Naomi. *Naomi* linamaanisha "wa kupendeza." *Elimeleki* alikuwa mumewe, linamaanisha "kuabudu." "Ibada ya kupendeza" ilikuwa ndiyo familia yake. Walikuwa na mtoto wa kiume, *Maloni*, ambalo linamaanisha "ugonjwa." Na *Kilion*, yule mwingine, alimaanisha "kuchoka, huzuni, majonzi." Hiyo hapo hiyo familia.

51 Ikawa njaa katika nchi ya Israeli. Na kosa la kwanza analofanya Myahudi, ni, kuondoka katika nchi hiyo. Mungu aliwapa nchi hiyo. Wakati Ibrahimu alipopewa nchi hiyo, Mungu alimwambia asiondoke katika nchi hiyo. Basi alifanya kosa aliposhuka kwenda Gerari, akaingia katika matatizo. Myahudi hapaswi kuondoka Palestina. Hapo ndipo mahali pake alipopewa.

52 Nao wamehamishwa, kote ulimwenguni. Na sasa wanarudi tena. Loo, ni hadithi nzuri sana tuliyo nayo hapa, asubuhi ya leo. Wanarudi.

53 Naomi alitoka kwa sababu ya njaa, Naomi na Elimeleki, nao wakaenda Moabu.

54 Sasa kupata usuli wa hadithi hiyo, ili kwamba, unaposikiliza, utaweza kuelewa vizuri ni kitu gani.

Sasa, Moab-. . . Wamoabu, walitokana na mtoto haramu, ambao walikuwa mabinti wa Lutu. Baada ya kuutoroka moto wa Sodoma, kwa neema ya Mungu, basi hao mabinti walimlewesha baba na kuishi naye, kama mke. Wakazaa mtoto. Ndipo mmoja wao alianzisha, na akaleta ta—taifa la Moabu, likidhaniwa kuwa Wakristo, lakini walikuwa wamechanganyana na upagani. Na, mnaona, kuiacha nchi ya ahadi, haidhuru ilikuwa mbaya jinsi gani, kuwa mgeni katika nchi nyingine, kulileta shida.

55 Na wakati wowote mwaminio anapotoka kwenye nchi aliyopewa na Mungu! Mara nyingi, katika siasa, uchaguzi huu unaokuja na kadhalika, mtu mzuri anaweza kuwa mtu mzuri,

naye atatangatanga atoke kwenye misingi hiyo. Kama mhudumu fulani nimjuaye, aligombea umeya wa jiji. Basi alipogombea umeya, akatoka katika misingi yake ya huduma, ndipo Shetani akampata.

56 Kama Mkristo yeyote akitoka kwa misingi hiyo. “Vema, nitashuka tu, usiku wa leo, niketi na hao wavulana kwenye chumba cha karata, kidogo. Sitafanya madhara yoyote. Nitachukua tu kinywaji kimoja kidogo.” Uko nje ya misingi yako. Rudi. Unajitia tu hatarini.

57 “Loo, wasichana wengine wote huvuta sigara. Nitajaribu moja tu.” Uko nje ya misingi yako. Msifanye hivyo. Kaeni kwenye nchi ya uenyeji wenu. Usifanye, “Kweli, kila mtu hapa, wananiita, ‘Mzee mpumbavu.’ Wananiita, ‘Mtindo wa kale. ’” Kaa hapo, hata hivyo. Hapo ndipo mahali pako. Dumu ndani ya Kristo.

58 Naomi, kwa sababu ya njaa, alitangatanga kutoka katika nchi hizo na kwenda Moabu, akitafuta chakula. Haikumpasa kufanya hivyo, kwa sababu wengine walikaa Yuda, Bethlehemu. Bethlehemu inamaanisha, *Betheli*, “nyumba ya Mungu,” nyumba ya sifa. Nao walikaa humo.

59 Basi alitangatanga akatoka pamoja na mumewe. Ndipo wanawe wawili wakaoa wasichana wa Moabu. Lakini ikiwa Mungu ameamua kitu fulani kifanyike, kitafanyika kwa vyovyote vile. Hiyo ndiyo sababu ninaamini kabisa katika kuchaguliwa tangu zamani, kujua mambo tangu zamani kwa Mungu.

60 Ndipo tunaona, kule, mauti iliikumba hiyo familia, nao wakaanza kurudi. Ua. . .Mvulana alikufa, wavulana wote wawili walifariki, naye baba akafa. Ndipo Ruthu akaanza kurudi, Orpa, na Naomi.

61 Sasa, ninataka kufananisha, asubuhi ya leo, Naomi, mama mkubwa, na kanisa la Othodoksi, kanisa la Othodoksi la Kiyahudi. Ruthu, Mmoabu, Mmataifa, akiwa Kanisa la Kikristo, Kanisa Jipya.

62 Nami ninataka kulikaribia, kutoka kwa awamu nne mbalimbali, Ruthu. Nimeziandika hapa. Ruthu, akiamua, akifanya uamuzi wake; Ruthu, akitumika; Ruthu, akipumzika; Ruthu, akizawadiwa. Tunaporudi: Ruthu, akifanya uamuzi; Ruthu, baada ya kufanya uamuzi wake, basi Ruthu anatumika; kisha Ruthu anapumzika; halafu Ruthu anazawadiwa.

63 Sasa, akiwa njiani akirudi, ulifika wakati, yeye akiwa ni mfano wa Kanisa, au Mkristo. Kwa kuwa, kila mtu anawakilisha taifa lote la Kikristo. Ulijua hilo? Wewe, katika matendo yako, jinsi utendavyo na kile ufanyacho, unawakilisha Mwili mzima wa Kristo. Unasema, “Lakini mimi ni mlei tu.” Hiyo haijalishi. Unapochukua jina hilo la Mkristo, unamwakilisha Kristo na Kanisa Lake. Unapaswa kuishi namna hiyo. Mnapaswa kuishi

kama waungwana, kama mama wa heshima. Kamwe usifanye mambo ya ulimwengu, kwa sababu macho yote ya Mbingu na dunia yako juu yako, kuwakilisha jambo hilo moja. Haijalishi u dhaifu jinsi gani, u mdogo jinsi gani, shikilia kichwa chako sawasawa, kwa sababu wewe ni Mkristo.

64 Sasa, Ruthu alikuwa mpagani, aliabudu sanamu, na pia Orpa. Nao walikuwa njiani, wakirudi na mama mkwe. Kwa sababu, alisikia, kwamba, kule Bethlehemu ya Yuda, kwamba Mungu alikuwa ameondoa lile pigo, na watu walikuwa na chakula. Alikuwa huko juu kama miaka kumi, kwa hivyo Edersheim anasema, "kama miaka kumi," mwanahistoria.

65 Na kurudi, mwenye huzuni (naye mumewe amekufa, watoto wake wamekufa), pamoja na wakwe zake wawili. Kisha akageuka, hapana shaka, na kuwatazama, akasema, "Kwa nini mwende na mimi? Sasa, hamwezi kufanya lolote ila kupata matatizo." Kasema, "Nasikitika kwamba mkono wa Mungu umenyooshwa dhidi yangu."

66 Ni mara ngapi Israeli wamefikiria hivyo, bila kujua kwamba yote yalikuwa ni mpango wa Mungu! Jinsi ukuta wa kuombolezea ulivyo tu nje ya Yerusalemu, ungali uko! Mawe ya kale ya hekalu, waliyaokota na kutengeneza ukuta. Nayo yamesuguliwa, kabisa, kwa machozi na kilio, kwa mikono ya Wayahudi, wakilia na kumsihi Yehova, "Yehova!" Hawatambui kuwa saa yao imekaribia sasa. Kuta za kuombolezea, "Mawe haya wakati mmoja yalilifanyia maskani lile Sanduku la Agano. Mfalme Daudi aliyaangalia mawe haya. Ee Yehova, uko wapi Wewe?" Unaona? Bila kujua kwamba hivi karibuni Mfalme wake atarudi, Mkombozi wake. Ilibidi watupwe nje, kwa kipindi kidogo.

67 Naomi alishangaa, "Kwa nini mkono wa Bwana umenidhulumu sana, wakwe zangu? Mungu amenitupa nje. Mimi nimetupwa. Sijui nimewahi kufanya nini, lakini mimi nimetupwa." Mnaona?

68 Mungu alikuwa akitekeleza mpango Wake. Kwa sababu, "Vitu vyote hufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu," haijalishi ni nini.

69 Alisema, "Rudi kwa mama yako, na kupata raha katika nyumba za mama zenu. Waume zenu wamekufa. Na ninyi ni wanawake wachanga, warembo. Rudini. Rudini mlikotoka. Huko mpate raha. Mungu awarehemu, kwa sababu mlikuwa wema kwa wafu. Na mumeishi vema tangu waume zenu walipokufa. Na mmekuwa wema kwangu, mwanamke mjane mzee asiye na mume, na mkanishikilia. Rudini, na Mungu awape raha katika nyumba yenu." Wakalia.

70 Akasema, "Kama. . .Mimi ni mzee. Nisingeweza kupata watoto wengine. Lakini kama ningepata mume na kumzaa mtoto, ingefaa nini? Kamwe msingemngojea mtoto huyo." Hiyo

hakika ilikuwa ndiyo sheria katika siku hizo. Kwamba kama ndugu akifa, au. . . na, ninii yake, ndugu huyo mwingine akiwa hajaoa, ilimbidi amchukue mkewe ili kumwinulia jina kaka yake aliyekufa. "Lakini, yeye," kasema, "msingemngojea, watoto hawa. Kwa hivyo, rudini mkajipatie raha katika nyumba za waume zenu. Rudi kwa mama yako."

71 Basi, Orpa, mfano wa kanisa vuguvugu ambalo liliwahi kuanza, mfano wa kanisa ambalo halitaenda safari yote. Alisema, "Hilo linasikika zuri sana." Kwa hivyo, akambusu mama mkwewe na kurudi tena. Huo ni mfano wa mwaminio vuguvugu, ambaye atamwamini Yesu kuwa ni Kristo, kisha ageuke na kurudi kwenye kitu ambacho ametoka. Kwa mtu ambaye atashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa, halafu ageuke, arudi nyuma. "Kama mbwa kwa matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaagaa kwake," kama Biblia ilivyosema.

72 Sasa, alirudi kwa miungu yake. Mara nyingi tunarudi kwa miungu yetu ya—ya mwanzoni. Labda tuna macho ya kutamani kitu kibaya. Tutarejea kwenye tamaa mbaya tena. Labda tuna sanamu za kunywa pombe, sanamu za kuvuta sigara, sanamu za uwongo, sanamu za kuiba, kila aina za sanamu; halafu kukiri na kubatizwa, na kisha kugeuka tena. Ni jambo la kusikitisha jinsi gani! Kumbukeni, halikutaja jina lake tena. Alitengwa kwa sababu ya uamuzi wake.

73 Kanisa vuguvugu, mwaminio vuguvugu, kwa kuwa kila mwaminio anawakilisha kanisa. Kila Mmarekani anawakilisha Marekani. Kila Mjerumani anawakilisha Ujerumani. Kila Mkristo anamwakilisha Kristo.

74 Hapa aligeuza mgongo wake, kurudi kwenye kitu alichotoka kwake. Jinsi ambavyo wanaume, hata wahubiri, wakati mwingine, watachukua njia ya Bwana, na unapozungumza nao juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu: "Upuuzi," wanamwondokea Huyo. Hao ni Orpa.

75 Waambie kuhusu Jina la Yesu Kristo, kwamba, "Hakuna Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo. Lolote ufanyalo kwa neno na tendo, fanya yote kwa Jina la Yesu Kristo, ikiwa hakuna Jina jingine chini ya Mbingu likupasalo kuokolewa kwalo." Ndipo Petro akasema, kwenye siku hiyo, Siku ya Pentekoste, "Mkitaka kuokoka, tubuni mkabatizwe, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu." Hivyo ndivyo zinavyoondolewa. Naye mtu, kwa sababu ya kupendwa na watu wengi, hawezi kushikilia Biblia juu yake. Lakini kwa sababu ya kupendwa na watu wengi, atalibusu Kanisa, ataubusu Ujumbe, atambusu Kristo, "kwaheri," na kurudi kule alikokuwa ametolewa. Orpa, vuguvugu, aliyetengwa.

76 Lakini, loo, jinsi ninavyompenda maskini Ruthu! Ilibidi afanye uamuzi. Ilinibidi kufanya uamuzi. Lazima ufanye

uamuzi. Kamwe hutatoka nje ya milango hii, asubuhi ya leo, bila namna fulani ya uamuzi. Hutaondoka kwenye chumba hiki, leo, ama ukiwa mwanaume bora zaidi au mwanamke, au mwanamume mbaya zaidi au mwanamke. Kulikataa, utakuwa mbaya zaidi. Itakuwa vigumu zaidi wakati mwingine, kwako kulifikia. Au, utatoka ukiwa bora zaidi.

77 Lilikuja shindano katika maisha yake. Inakuwa shindano katika maisha ya kila mtu. Basi Ruthu ilibidi afanye uamuzi. Kwa hiyo, Biblia ilisema kwamba mama mkwe wake alimwambia, "Rudi kwa miungu wako kama vile dada yako alivyofanya. Rudi nyuma kama vile huyo mwenye uvuguvugu alivyofanya. Kwa nini usirudi nyuma."

78 Mhubiri wa Injili, "Ikiwa unataka kwenda, nenda." Mhubiri halisi na wa kweli atakayeliweka mbele ya darasa la watu, "Ninyi jiamulieni. Simameni kwa miguu yenu." Mwenye uvuguvugu, asiye na msimamo, mnyonge, hatasema hivyo. Lakini mtumishi halisi wa Mungu ataliweka mkononi mwako, "Fanya uamuzi wako."

79 Ruthu akasema, "Nitaenda uendako. Watu wako watakuwa watu wangu. Mungu wako atakuwa Mungu wangu. Uishipo, nitaishi. Pale utakapokufa, nitakufa. Na mahali utakapozikwa, nitazikwa." Huo hapo uamuzi halisi.

80 "Bwana, nitakuchukua kama Mwokozi wangu. Kama Biblia inasema, 'Tubuni mkabatizwe, katika Jina la Yesu Kristo,' hilo nitafanya. Ikiwa Biblia ilisema 'lazima nipokee Roho Mtakatifu,' hilo nitafanya. Ikiwa Biblia inaniambia, 'Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, hilo nitaamini. Nitaichukua Biblia na Mungu, kwa yale aliyoandika na jinsi alivyo Yeye, haidhuru mtu yeyote mwingine alisema nini." Huyo hapo Ruthu halisi.

81 Alifanya uamuzi wake. Ilibidi ama arudi nyuma au aende mbele. Tunasimama kwenye misingi hiyo hiyo, asubuhi ya leo, kurudi nyuma au kwenda mbele. Msirudi nyuma kamwe. Hima twendeni mbele.

82 Moja kwa moja wakaingia katika nchi ya ahadi, katika nchi ya watu wageni. Ruthu, mfano wa mwaminio sasa. Kitu gani? Mwaminio ni nini? Wakati mwanamke ama mwanamume anapotoka, huyo mtu kutoka ulimwenguni, huingia miongoni mwa waaminio Wakristo. Wanawake waliozoea kuvuta sigara, kunywa pombe, na kucheza karata kwenye vyama, na kadhalika, na kuwa na kila aina ya vitu vya kupendeza, na kama aina fulani ya "ndege anayechachatika," lakini sasa amebadilika. Ameamua kwenda na Mungu. Sasa anakuja kwa watu ambao hawaamini upuuzi wa namna hiyo. Yeye ni mgeni. Lazima atembee kama msafiri. Hajui mila zao. Zote ni ngeni, kwake. Hajui afanye nini. Hivyo ndivyo ilivyombidi Ruthu kufanya. Hivyo ndivyo huna budi kufanya. Hivyo ndivyo inanibidi kufanya.

83 Nilipompokea Kristo, nilifukuzwa nyumbani kwangu. Nilipompokea Kristo, marafiki wangu wa kiume, marafiki wa kike, kila mtu, walinitupa chini. Nikashuka chini pamoja na kundi la wazee ambao walikuwa na Roho Mtakatifu na kumwamini Mungu, nikimtumikia Yeye. Wasichana, waliokuwa huko chini katika kanisa hilo, walikuwa tofauti na wasichana ambao nilikuwa nikiambatana nao. Walionekana tofauti. Walifanya tofauti. Walikuwa wa kipekee, nami niliwaogopa. Walikuwa watu tofauti.

84 Hivyo ndivyo ilivyombidi Ruthu kufanya. Alilazimika kutoka kwa watu wake mwenyewe, kwenda kwa watu wengine. Aliongoka. Alifanya uamuzi.

Na wewe fanya uamuzi. Huna budi kufanya chaguo lako. Unataka kurudi kwenye mambo ya ulimwengu, au unataka kuendelea na Mungu?

85 Je, unataka kufanya kama ulimwengu na wengine wote? Basi mbusu Kristo "kwaheri" na urudi nyuma.

Lakini ikiwa unataka kuchukua njia yako na wachache wa Bwana waliodharauliwa, shikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Bila kujali yale walimwengu wengine wasemayo, wewe shikilia papo hapo. "Mungu alisema hivyo. Ni kweli. Ninaiamini, ingawa siwezi kulidhihirisha maishani mwangu. Mungu alisema hivyo. Ninaiamini. Ninashikilia papa hapa."

86 Hivyo ndivyo alivyomfanyia Naomi. "Sitakuacha. Nitaenda uendako. Watu wako watakuwa wangu. Jinsi watendavyo, ndivyo nitakavyotenda. Jinsi wafanyavyo, ndivyo nitakavyofanya. Walacho, ndicho nitakachokula. Pale utakapokufa, nitakufa. Pale utakapozikwa, nitazikwa. Na Bwana anitendee zaidi ikiwa nitashindwa popote." Huo ni uamuzi dhahiri kabisa. Mungu anataka maamuzi dhahiri kutoka kwa Kanisa Lake.

87 "Vema, Bwana, ikiwa utanibariki tu na kunifanyia *hivi*, nitafanya *hivi-na-vile*." Huo sio uamuzi.

88 "Mungu, sijali utafanya nini nami, nitaenda hata hivyo. Nikifa, sawa. Niishi au nife, chochote! Wakinicheka, wanidhihaki, haileti tofauti yoyote, nitakwenda hata hivyo." Huo ni uamuzi dhahiri, kama vile Rebeka alivyofanya kabla hata hajamwona Isaka.

89 Wazazi wake walisema, "Hebu msichana ajibu. Msichana, ni mtu mzima, acha ajibu."

90 Alisema, "Nitaenda." Uamuzi dhahiri, uliofanywa haraka. Aliushikilia. Hivyo ndivyo Ruthu alivyofanya. Orpa akarudi.

91 Wakaendelea na safari. Ruthu, moyoni mwake, pasipo kujua mahali alipokuwa anaenda, lakini mfano wa Kanisa. Sisi ni wageni, kama Ibrahimu. Wasafiri katika nchi ya ugeni, miongoni mwa watu wageni.

Basi akaendelea, na mwishowe akaingia chumbani na mahali ambapo Naomi alikuwa akimleta. Basi alipata nini? Kila mtu akimpigapiga mgongoni na kusema, "Ruthu, tuna furaha kuwa nawe hapa chini"? Alikuta ugomvi. Alikuta kitu kiovu. Alikuta matatizo.

92 Na wahubiri watakaokuambia kwamba, "Ma—maisha ya Kikristo ni raha mstarehe," ama anakudanganya au hajawahi kupokea tukio hilo yeye mwenyewe. Ulimwengu unakuchukia. Na watu watakuchukia. Lazima ushike njia ya wachache wa Bwana waliodharauliwa, na kuchekwa, kudhihakiwa, au chochote kile. Lazima uwe tofauti. Umezaliwa na Taifa lingine.

93 Mke wangu . . . Kama ni—nitakavyonukuu tena; inaonekana ni vizuri sana kunukuu. Aliniuliza, "Kwa nini wanawake Wakristo hawavai nguo hizo kama wanawake wengine?" Nikasema . . . Akasema, "Sisi sote ni Wamarekani, sivyo?"

94 Nikasema, "La, bwana."

95 "Vema, sisi ni nini?"

96 Nikasema, "Sisi sio Wajerumani, Wafaransa, Wabeljiji, Waswisi, Mwafrika, au Wamarekani, au wowote wale."

97 "Lakini sisi ni nini?"

98 Nikasema, "Sisi ni Wakristo." Mmarekani hufanya kama Mmarekani, Mjerumani hufanya kama Mjerumani, kwa sababu hiyo ni roho yao ya kitaifa. Nasi tuna Roho wa kitaifa. Huyo ni Roho Mtakatifu anayetoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, nawe unatenda namna Hiyo. Hukufanya uenende kama wanavyofanya Huko, kwa sababu wewe ni wa Ulimwengu mwingine.

99 Tunaishi Marekani, hiyo ni kweli. Hiyo ni sehemu ya mwili. Lakini roho inayotuongoza, tabia yetu, inatoka Juu. Tunaishi kutoka Juu kwa sababu tumezaliwa kutoka Juu. Wakristo wote wanatoka Juu. Yesu alisema, "Mimi si wa chini. Ninatoka Juu. Kama ningalitoka chini, raia Wangu wangenipigania. Lakini Ufalme Wangu ni wa huko Juu." Ndivyo alivyo kila mtu aliyezaliwa na Ufalme wa Mungu, yeye anatoka Juu.

100 Sasa, tukiangalia sasa. Tunapoendelea, tunawakuta wakiudhika. Je, hapo ndipo ulipofikia, wakati ulipompata Roho Mtakatifu? Hakika nilipafikia. Nilipafikia. Kudhihakiwa, na kila kitu.

101 Halafu, angalia, maisha yalikuwa ni magumu kwake. Na ni magumu ukiisha kuwa Mkristo. Kwa sababu unapaswa kujirekebisha kutoka kwa maisha ya aina moja, ya tafrija na raha za ulimwengu, kuingia kwenye maisha mengine, ya kujitolea kwa Mungu. Lazima ujirekebishe, upande *huu*.

102 Basi ilimlazimu Ruthu kujirekebisha kutoka kuwa kwenye nchi ya chakula tele, na kila kitu kuheshimiwa, kuingia kwa watu waliokuwa wakimcheka, wakimdhihaki, hadi kwenye nchi aliyokusanya masazo shambani apate chakula. Akayaweka

kwenye skafu yake na kuyapeleka nyumbani. Na kuyapepeta na kuoka mkate, naye na mama mkwe wake wakaila.

103 Alipokuwa huko, walikuja kujua, wakati alipokuwa akiokota masazo, au akienda kuokota masazo . . . Sasa, alifanya uamuzi wake. Hiyo ilikuwa ni yeye akiamua.

104 Sasa, jambo lingine analopaswa kufanya ni kutumika.

105 Na hivyo ndivyo Kanisa halina budi kufanya. Kanisa, baada ya kufanya uamuzi wenu, inawapasa kutumika. Mtumikie Mungu kulingana na mpango Wake, kulingana na ramani Yake. Huna budi kumtumikia Mungu.

106 Ruthu, akifanya uamuzi. Sasa, Ruthu, akihudumu chini ya uamuzi wake. Sasa angalieni kwa dakika moja. Sasa yeye anaenda shambani, kuokota masazo.

107 Sasa, mama yake alimwambia; ambapo, Agano la Kale likiliambia lile Jipya, unajua. Mama yake alimwambia, akasema, "Tunaye jamaa, na jina lake ni Boazi. Yeye ni tajiri. Naye ni jamaa wa karibu. Nenda shambani mwake. Na labda . . . Usiende kwenye shamba lingine; nenda shambani mwake."

108 Jinsi Roho Mtakatifu anavyotuambia tusiende kando kwenye aina fulani ya ki—kitabu cha kanisa, aina fulani ya katekismo, lakini twende Shambani mwa Mungu, Agano la Kale, Biblia. Usiseme, "Vema, tutasema *hivi*. Na tutasema *hivi* kwa ajili ya sala. Tutakuwa na *hii*." Kaa mumo humo Shambani. Nenda moja kwa moja ndani Yake, maana Yeye ndiye Jamaa wa karibu.

109 Neno la Mungu, Agano la Kale, ni Jamaa wa karibu kwa lile Jipya. Kanisa la Kale ni mama wa Kanisa Jipya, unaona, Mkristo, mwaminio. "Usiende kwenye shamba lingine. Kaa mumo humo shambani mwake. Na labda, siku moja, huenda ukapata neema kwake."

110 Basi siku moja, wakati akiwa shambani, huyu kijana tajiri, jina lake Boazi, mtawala, tajiri, alipitia hapo, naye akamwona. Loo, alipomwona, akampenda. Alifikiri alikuwa mwanamke mzuri sana. Alipenda tabia yake. Mnakumbuka, alisema, "Najua, halafu watu wanajua, ya kuwa wewe ni mwanamke mwadilifu." Alifanya uamuzi wake, safi na wazi. Akarudi moja kwa moja, akaishi sawasawa na yale aliyosema angefanya.

111 Vinginevyo, leo hii, wanasema, "Tunajua kwamba wewe ni Mkristo. Tunajua kuwa wewe ni mtu wa Mungu, maana hakuna mtu anayeweza kufanya miujiza hii isipokuwa Mungu awe pamoja naye."

112 Hivyo ndivyo Nikodemo alivyomwambia Yesu, akasema, "Rabi, tunajua kuwa wewe ni mwalimu uliyetoka kwa Mungu. Hakuna mtu awezaye kuyafanya mambo uyafanyayo wewe

isipokuwa Mungu yu pamoja naye." Wakati, angeweza kumwona Yeye ameketi pale na kuyatambua mawazo ya mioyo yao hasa.

113 Mwanamke aligusa vazi Lake. Akageuka, akasema, "Nani alinigusa?" Wote wakakana. Akaangalia tena katika kusanyiko na kusema, "Wewe, unayetokwa na damu hapo, imani yako imekuponya."

114 Kasema, "Hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo isipokuwa Mungu awe pamoja naye. Tunajua Wewe umetoka kwa Mungu. Hatuwezi kukukubali, kwa sababu tutafukuzwa kanisani." Mnaona?

Mzabibu huo uliopandikizwa, Ndugu West, kama tulivyokuwa tukizungumza jana usiku, watakutupa nje. "Lakini, chini moyoni mwetu, tunajua umetoka kwenye Mzabibu asili." Kristo ndiye Mzabibu; sisi ni matawi. "Tunajua, kwa sababu tunaona Uzima ule ule ulioko ndani ya Mungu, uko ndani Yako."

115 Huo ndio Boazi alikuwa ameona kwa Ruthu, uamuzi huo dhahiri, uadilifu huo wa mwanamke aliyesimama pale. Naye akampenda.

116 Sasa, nawatakeni muone. Naomi, lile kanisa la zamani, akaanza kumwelezea Ruthu sheria zote kuhusu dini yake, kama vile Agano la Kale lilivyo kivuli cha lile Jipya. Sasa, nawatakeni mwipate hadithi hii papa hapa.

117 Sasa, nataka kuonyesha vivuli. Agano la Kale linalielezea lile Jipya, ikiwa utalisoma tu, kwa maana ni kivuli cha lile Jipya. Sasa, kama nilikuwa nikielekea kwenye ule ukuta, na sikuwa nimejiona mwenyewe, na nikione kivuli changu, ningejua, ningekuwa na dhana ya sura yangu. Na ikiwa (wewe) hujui Agano Jipya ni nini, soma la Kale nawe utaona kivuli chake. Unaona? Ndipo basi Agano Jipya linapoingia, unasema, "Mbona, hakika, hili Ndilo." Kitabu cha Waebrania, tukirudi nyuma, Paulo akikielezea.

118 Sasa, angalia kwa makini sasa. Wakati Ruthu aliposema, au. . .Naomi akamwambia Ruthu, kasema, "Sasa, yeye ni wa mbari yetu. Na ikiwa unaweza kupata neema machoni pake, utapata raha." Loo, jamani! "Ikiwa unaweza kupata neema, utapata raha." Boazi alimwakilisha Kristo, Mtu mwenye mali, mrithi wa vitu vyote, Bwana wa mavuno. Loo, jamani! Jinsi, wakati Boazi alikuja amepanda huko nje, ndani ya gari lile, akiangalia kote shambani, basi macho yake yakatua juu ya Ruthu! Alikuwa ni bwana. Alikuwa bwana wa mavuno. Naye akapata neema machoni pake.

119 Hivyo ndivyo Kanisa lifanyavyo, siku hizi. Wakati Bwana wa mavuno akipita, Yeye haangalii jengo kubwa, minara mikubwa, kwaya zilizofunzwa vizuri. Anatafuta watu binafsi, wanaume na wanawake ambao wamejitolea na kufanya uamuzi dhahiri kwa Kristo, waliojiweka wakfu kwa utumishi Wake.

"Mungu, ninaliamini, kila Neno Lake. Wakati Neno Lako likisema chochote, mimi hukaa moja kwa moja na Hilo. Hilo ni Neno Lako. Ninaliamini, kila Neno." Hicho ndicho anachotafuta; Bwana wa mavuno. Huyo ndiye anataka kuwapa, Roho Mtakatifu, kwa wale ambao wana njaa na kiu. "Heri ninyi wenye njaa na kiu, kwa maana mtashibishwa." Anajaribu kupata Kanisa hilo, leo.

120 Sasa, basi, Ruthu aliombwa kufanya jambo ambalo lilikuwa la aibu, bali alikuwa tayari kwa sababu alikuwa amefanya uamuzi wake. Ni mfano jinsi gani wa mwaminio! Ni mfano mkamilifu jinsi gani!

121 Naomi, lile kanisa la kale, akasema, "Shuka uende, usiku wa leo. Ni msimu wa shayiri." Loo, ni wazo zuri jinsi gani tungeweza kutegemea hapo hapo!

122 Naomi na Ruthu walikuja kwenye msimu wa shayiri. Msimu wa shayiri ulikuwa msimu wa mkate, msimu ambao mkate mpya ulikuwa ukitolewa. Nalo Kanisa, katika siku hizi za mwisho, kupitia miaka elfu mbili ya mafundisho ya kipagani na kadhalika, limekuja kwenye msimu wa shayiri, na Maisha mapya, Mkate mpya, asali kutoka Mbinguni. (Russell, zungumza juu ya mkate wa ganda la asali!) Huu Ndio, Mkate kutoka Mbinguni. "Mimi ndimi Mkate wa Uzima. Baba zenu walikula mana, nao wamekufa. Lakini mimi ndimi Mkate wa Uzima utokao kwa Mungu, Mbinguni. Mtu akiula Mkate huu hatakufa kamwe." Nalo Kanisa katika siku hizi za mwisho hapa, linaletwa, sasa hivi, kwenye msimu wa shayiri.

123 Ruthu, Mmataifa, aliyetengwa, akafukuzwa, ameingizwa ndani, ili akubaliwe kama Bibi-arusi. Kristo aliingia, kwenye msimu tu wa shayiri.

124 Alisema, "Sasa jivike mavazi yako." (Sio, "Vua mavazi yako.") Ni kinyume jinsi gani leo! "Jifunge mavazi yako, utakapokwenda kumlaki. Anaenda kupepeta shayiri, usiku wa leo. Shuka ujivike mavazi yako. Jifunike, ili kumlaki."

125 Siku hizi, wanataka kujifunua. Jifunike. "Shuka, kwa sababu anapepeta shayiri. Na halafu uangalie mahali anapolala." Ulifanya hivyo? Juu ya Golgotha. Miaka mingi iliyopita, nilipaangalia moyoni mwangu mahali alipoyaweka maisha Yake, apate kunichukua. Paangalie mahali anapolala. Angalia mahali alipolala. Hilo ndilo kila mwaminio anapaswa kufanya. Angalia aliyokufanyia. Ujumbe wa Jumapili iliyopita, juu ya *Ziara Ya Kalvari,* angalia aliyokufanyia.

126 Alisema, "Angalia mahali anapolala. Ndipo atakapojilaza chini kulala usingizi, kupumzika, nenda ujilaze miguuni pake." Sio kichwani mwake; miguuni pake, kutostahili. "Kisha uchukue blanketi aliyokuwa amejifunika nayo, ukajifunike nayo." Loo! Mnaiona? Loo, jamani! Najua mnaweza kudhani mimi ni mlokole. Lakini huyo ananifaa tu vizuri, huyo Roho

wa Mungu. Angalia mahali alipolala, Kalvari; ambapo alilala kaburini; huko Gethsemane. Angalia, na utambae hadi miguuni Pake. Lala chini pale na ufe, wewe mwenyewe, kwa ninii yako . . . Haya basi. Jifunike, kabisa, na sketi Yake. Alisema, "Sketi," ndivyo alivyoiita.

127 Naye Ruthu akasema, "Usemayo, nitayafanya."

128 Loo, ni uamuzi dhahiri jinsi gani kwa mwaminio! "Yale Biblia isemayo, hayo nitafanya. Anasema, 'Tubuni mkabatizwe, Jina la Yesu Kristo,' nitafanya hivyo. Kama likisema, 'Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili,' nitafanya hivyo. Ikiwa inasema, chochote ilichosema, 'Yesu Kristo yeye yule jana, milele.' Inachosema nifanye, nitafanya." Unaona, Kanisa likiyachukua maagizo Yake kutoka kwa Neno. Likajilaza chini.

129 Sasa, kumbuka, hiyo ilikuwa ni aibu kwa mwanamke huyo mjane mchanga kulala kando ya mtu huyu, miguuni pake. Aibu, kwa ulimwengu wa nje.

130 Loo, mnaweza kulivumilia? Hii hapa. Angalieni. Angalieni. Jambo ndilo hili. Kanisa, msichana, kijana mwanamume, mzee au kijana, wanaombwa kujitenga na ulimwengu, na kuingia mahali fulani, Ufalme wa Roho Mtakatifu, hiyo ni aibu kwa ulimwengu. Moyoni mwao wenyewe wanajua yote yanahusu nini. Lakini, kwa ulimwengu, wanakuwa walokole. Wanakuwa mtakatifu anayejibingirisha ama kitu kama hicho, jina fulani la aibu. Lakini Kanisa linaombwa kufanya hivyo. Je, uko tayari kupaangalia mahali hapo, na kujilaza chini, uache ulimwengu ukuite chochote watakacho?

131 Ule wimbo wa kale, tuliozoea kuimba:

> Nimeanza kutembea na Yesu peke yake, (Unaona?)
> Mto wangu, kama Yakobo, ni jiwe;
> Nami nitachukua njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa;
> Nimeanza na Yesu. Ninapita.

132 Jambo ndilo hilo. Nitalipa gharama, hata wengine wafanye nini. Ikimaanisha fedheha, ikiwa inamaanisha kupoteza makazi, kupoteza—kupoteza familia, wenzako wote, marafiki wa kike, marafiki wa kiume, vyovyote inavyomaanisha, nitaenda peke yangu. Nitachukua njia. Kama jirani yangu anasema mimi ni "mtakatifu anayejibingirisha, mpentekoste, au mlokole," Sijali wasemacho. Haileti tofauti hata moja kwangu. Nimeanza. Nimeweka uamuzi wangu wazi, na ninapita.

133 Sasa, huyo ndiye peke yake angeweza kumpa raha, kutoka kwenye mashamba ya uchovu ya kuokota masazo. Loo, ilikuwa tamu sana wakati, Boazi, wakati alipompata huko shambani. Siwezi kukosa hii. Boazi alimkuta huko nje shambani. Alisema, "Angalia." Akasema, "U nani wewe?"

Sema, "Jina langu ni Ruthu."

"Loo, yule Mmoabu aliyekuja kukaa pamoja nasi."

"Naam."

134 "Nimesikia habari zako. Huendi kwenye mashamba mengine." Aha! Ninapenda hiyo. "Usianze kutangatanga kwenye misheni. Kaa hapa hapa shambani mwangu. Kaa na walio wangu." Alimpenda. "Kaa hapa. Kaa pamoja nami. Usiende kutangatanga mahali mahali. Kaa hapa."

135 Ikiwa unauamini Ujumbe, ning'inia Kwake. Unaona? Haidhuru itagharimu nini, kaa nao. Endelea moja kwa moja. "Ikiwa inamaanisha, achana na *hili, lile,* au lile *lingine*. Na inanilazimu kuachana na kunywa pombe, inanibidi kuacha wizi wangu, kusema uwongo. Nitadumu nao moja kwa moja." Unaona?

136 Ndipo ikasemwa tena, akasema, "Sasa, hawatakusumbua, kwa sababu nimewaagiza vijana wasikuguse." Amina. Ninapenda hiyo, ulinzi wake. Ni nani aliyesema hivyo? Bwana wa mavuno.

137 Iweni waangalifu. "Msiwaguse masihi Wangu. Msiwadhuru manabii Wangu." Hiyo ni kweli? "Kwa kuwa amini, nakwambia, yakufaa sana kufungiwa jiwe la kusagia shingoni mwako, na kutoswa baharini, kuliko kumkosesha aliye mdogo zaidi wa hawa, wadogo Wangu." Hiyo ni kweli? "Usiwakoseshe hata kidogo."

"Nimewaagiza wasikuguse." Loo, angalia ulimwengu huo! Ni mtesaji. Saa yao imekaribia.

138 Kisha akawaendea wale vijana, hao wengine. Alisema, "Sasa, anakusanya masazo kwa ajili ya uhai. Sasa, nataka ninyi wavunaji. . . nyinyi malaika," kwa maneno mengine. Ndivyo walivyo. Kasema, "Nawatakeni nyinyi malaika, ninyi wavunaji, mara kwa mara, mwangushe konzi moja, makusudi." Loo! "Msiache iwe ya kuchosha sana kwake. Lakini kila mara kwa mara, acheni asikie Ujumbe mzuri. Acha nguvu nzuri za Roho Mtakatifu zimfunike, mara kwa mara, kumfanya ajue kwamba ningali niko. Fanya namna fulani ya uponyaji miongoni Mwake. Onyesha namna fulani ya ishara au ajabu, apate kujua kwamba Niko miongoni Mwake." Hivyo tu.

139 Hivi hampendi kupata makonzi hayo? Natumai tutapata kiasi asubuhi ya leo, sivyo? Konzi ya shayiri mpya. Bwana afanye kitu alichokuwa akifanya. Kitu ambacho tunajua Yeye hufanya. Yeye ni Bwana wa Mavuno. Yeye Ndiye wa pekee anayeweza kuangusha hiyo konzi. "Nawaagiza malaika washuke kwenye mkutano huo asubuhi ya leo. Ninataka wafanye jambo fulani, fulani. Nimewaagiza, na watalifanya." Loo, jamani.

140 Sasa, hapa, ilimbidi achukue sehemu ya aibu, kulala chini, kuitwa chochote alichotaka. Angeweza kuitwa kahaba, unajua.

Angeweza kuitwa mwanamke mwenye sifa mbaya, hata hivyo hakuwa. Naye alikuwa akifuata kikamilifu sheria ambazo alikuwa amepewa. Kwa hivyo yeye akashuka na kujifunika, kwa kifuniko alichokuwa amejifunika. Angeenda wapi? Kaburini. Angeenda wapi? Ambapo alikuwa akipumzika.

141 Hapo ndipo nilipoipata.

> Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu,
> Huko chini kwa ajili ya kusafishwa na dhambi nililia,
> Huko moyoni mwangu Damu ilitumika.
>
> Kuna Chemchemi iliyojaa Damu
> Inayotoka kwenye mishipa ya Imanueli;
> Ambapo wenye dhambi, wakijitumbukiza chini ya hayo mafuriko,
> Hupoteza waa lao lote la dhambi.

142 Angalia mahali alipojilaza chini, nawe ujilaze chini hapo pamoja Naye. Je, uko tayari kwenda Kalvari, asubuhi ya leo, kama nilivyosema Jumapili iliyopita? Umepaangalia mahali hapo maishani mwako? Je, umefika mwenyewe mahali Yesu aliposulubiwa?

143 "Loo, tunathamini hilo." Lakini vipi kuhusu kusulubiwa kwako? Uko tayari kuchukua njia pamoja na jina la fedheha, kama mtakatifu anayejibingirisha, shupavu wa dini, au chochote, chochote itakachogharimu?

144 Je, umeangalia mahali hapo, upate kwenda huko na kulala pamoja Naye, useme, "Bwana, mimi hapa"? Halafu nini? Vuta kifuniko hicho hicho kilichokuwa juu Yake, ukajifunike.

145 Mwanamke mmoja wakati mmoja alimwambia Bwana wetu, "Bwana, wajalie wanangu wawili, kwamba mmoja ataketi mkono wa kuume, na mkono wa kushoto, katika Ufalme."

146 Alisema, "Mnaweza kukinywea kikombe ninachokinywea?" Hayo ni yale mateso makali.

"Naam."

147 "Na mnaweza kubatizwa na ubatizo ambao nimebatizwa nao?" Akajilaza chini, akavuta kifuniko kile kile juu yake.

148 Eliya alitwaliwa juu. Naye Eliya akatupa chini kifuniko kile kile alichokuwa nacho, ili kumfunika Elisha kwa sehemu maradufu ya Roho yake. Kitu kile ile, sehemu maradufu tu. Nguvu zile zile; si zaidi. Si zaidi, si kubwa zaidi; sehemu maradufu tu Yake.

149 Kama vile Musa, wakati alipokuwa amechoka, baba mkwe wake alimwambia, akasema, "Unajichosha. Omba Mungu achukue Roho yako na kuiweka kwa wengine." Naye akaomba.

150 Ndipo Yeye akaichukua hiyo Roho na kuiweka juu ya wengine sabini nao sabini wakaanza kutabiri. Hawakuwa na

nguvu zaidi. Walikuwa na mitambo zaidi. Hivyo tu. Kitu kile kile, walikuwa tu na mitambo zaidi.

151 Ndivyo ilivyo, leo. Mtu mmoja hawezi kulifanya. Mungu ana mitambo Yake ikifanya kazi kila mahali, bali ni nguvu zile zile; nguvu zile zile, Roho Mtakatifu yeye yule, Yesu yeye yule.

152 Sasa, akachukua blanketi, Roho Mtakatifu, alipokufa kwa nafsi yake. Akaangalia mahali alipofia, ambapo alijilaza chini kupumzika. Kisha akajilaza chini, akachukua blanketi iliyokuwa juu yake na kuivuta juu yake. Ndipo yule mtu akaamka, akasema, "Nani yuko hapo?" Alisema . . . Alisema, "Mimi ni Ruthu, Mmoabu, mjakazi wako."

153 Basi akasimama. Akasema, "Ninaona na kujua wewe ni mwanamke mwema." Amina. Loo! Hivi hilo halisababishi mitetemo midogo nafsini mwako? "Wewe ni mwanamke mwema."

154 Basi alijibu nini? "Lakini wewe ni jamaa wa karibu." Amina. "Wewe ni jamaa wa karibu. Unaweza kunifanyia. Unaweza kunipumzisha. Nimekuja hapa na kujilaza hapa, sio kuwa mwanamke mtovu wa uadilifu. Nimejilaza hapa, sio kwa kujionyesha; kuwaonyesha watu ninaweza kunena kwa lugha, kuonyesha watu ninaweza kucheza katika Roho, na kuwaonyesha watu ninaweza kupaza sauti. Lakini nimekuja hapa kwa sababu wewe ni jamaa wa karibu. Sio kuonyesha kuwa naweza kufanya kitu kikubwa; lakini wewe ni mbari yangu. Nimekuja kwa sababu wewe ni jamaa wa karibu, na wewe ndiye pekee unayeweza kunikomboa."

155 Mnaona mtazamo wa—wa mwongofu kwa Kristo, kwa Kanisa? Mnaona? Mnaona? "Wewe ni jamaa yangu wa karibu."

156 Naye akasema, "Wewe ni mwanamke mwema. Na mimi ni jamaa yako wa karibu. Sasa, jifunike. Lala hata asubuhi." Whiu! "Jifunike tu na blanketi hilo. Mimi ni wa mbari yako. Lala hapo hata asubuhi, ukipumzika." Amina. Amina. "Mimi ni jamaa yako wa karibu. Pumzika!" Amina.

157 Kulipokucha, mapema kabla ya mapambazuko ya siku, alikusanya lundo kubwa la shayiri, vipimo sita, naamini ndivyo, na kuiweka kwenye maskini shela ya—yake akaenda nyumbani.

Ndi—ndipo Naomi akasema, "Binti yangu."

158 Baada ya kuinuka kutoka madhabahuni, na kurudi nyuma. "Sasa itakuwaje, mama? Itakuwaje sasa?" Amina.

159 "Tulia." Amina. "Tulia, Ruthu, kwa sababu mtu huyo hatatulia hata atakapolipa gharama kamili ya ukombozi." Amina. Amina. Papo hapo ndipo ninaposimama. Amina. Hataridhika mpaka ametimiza gharama yote ya ukombozi, kukukomboa, kila kitu ulichopata kupoteza, kila kitu ulichokuwa.

160 Sasa kumbukeni sheria ya ukombozi, tunapokaribia kufunga, hadi mwisho wa ibada. Sheria yote ya ukombozi ni hii, kwamba, kabla ya mtu kuweza kuikomboa mali iliyopotea, ilibidi awe wa jamaa aliye karibu zaidi. Na jambo la pili, ilibidi awe mtu mnyofu, mtu mwenye haki, kufanya hivyo. Halafu ilibidi awe na mali ya kutosha, kufanya hivyo. Halafu ilibidi atoe ushuhuda hadharani kwamba alikuwa amefanya hivyo. Na tangu wakati huo na kuendelea, ilikuwa ni mali yake.

161 Basi sasa angalieni. Boazi alimwakilisha Kristo. Sasa, Ruthu aliwakilisha Kanisa, wewe, mwaminio. Na sasa, Mungu, katika Agano la Kale, njia pekee ambayo angeweza kuja kukomboa kile kilichokuwa kimepotea, ilibidi Mungu afanyike mbari ya mwanadamu. Na njia pekee ambayo Mungu angeweza kuwa wa mbari ya mwanadamu, ilikuwa ni kuwa mmoja wao. Amina.

162 Ninatofautiana na Billy Graham, juu ya watu watatu mbalimbali katika Uungu, au mwalimu mwingine yeyote wa utatu, juu ya hilo. Ninaamini katika utatu, hakika, lakini sio kwa njia hiyo, hao wakiwa watu watatu. Hao ni Mmoja. Hadithi hiyo pale, peke yake, haikuwa na kitu kingine ila hicho, ingelithibitisha.

163 Mungu alifanyika mwanadamu. Ilibidi awe wa mbari. Wala asingeweza kuwa Mungu, na sisi wenye dhambi, viumbe vya uumbaji Wake, viumbe umbaji vya uumbaji Wake, maana hatungeweza kuwa wa mbari moja huko. Kwa hivyo, Mungu alifanyika mwanadamu, kusudi mwanadamu aweze kuwa Mungu, awe Mungu. Amina.

164 Sisi, tukiwa wanadamu, wenye dhambi, Mungu akafanyika mwenye dhambi, akajitwika dhambi zetu. Pasipo kujua dhambi, hata hivyo alikuwa mwenye dhambi kwa sababu dhambi zetu ziliwekwa juu Yake. Ili kwamba sisi. . . Yeye alifanyika mimi, nipate kuwa Yeye. Unaona? Akawa mwenye dhambi, nipate kuwa mwana wa Mungu. Yeye akawa mwenye dhambi, upate kuwa mwana wa Mungu. Na sasa sisi ni wana na binti za Mungu, kwa sababu Mungu alifanywa mbari yetu wakati alipochukua umbo la mwili wetu, akazaliwa na mwanamke. Mungu! Sio mtu mwingine; Mungu, Mwenyewe.

165 Timotheo wa kwanza 3:16 ilisema:

> . . . *bila ubishi siri ya utauwa ni kuu:* kwa kuwa *Mungu* alidhihirishwa *katika mwili,* . . . Mungu!
>
> *Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye Neno alifanyika mwili,* . . .

166 Neno, alifanywa mwanadamu, akawa wa jamaa. Akawa mtu. Loo! Alifanyika kifo, ili kwa kifo Chake niweze kuwa Uzima. Alifanyika mwenye dhambi, ili kwa haki Yake nipate kuwa. . . kupata Uzima. Akawa maskini, ili mimi, kwa umaskini Wake,

niweze kuwa tajiri. Alifanyika kile nilichokuwa, ili kwamba mimi, kwa neema Yake, niwe kile alicho Yeye. Loo, jamani! Basi, nena kuhusu nguvu za Mungu! Sasa, hiyo ni Maandiko kabisa. Na hivyo ndivyo Maandiko yasemavyo.

167 Ili tuweze kuwa...Je, ni upendo gani, ambao Baba amemwaga juu yetu, amemwaga juu yetu, kwamba sisi tuliokuwa wenye dhambi, wageni, mbali na Mungu, tupate kuvutwa karibu na Mungu, hata tunafanyika wana na binti za Mungu, sio watumishi. Kanisa la Mataifa kamwe si mtumishi. La, bwana. Kanisa la Mataifa ni mwana na binti. Ninyi ni wana na binti za Mungu, ambao mumempokea Roho Mtakatifu. Sasa, ikiwa wewe ni kundi la Orpa, na ukageuka? Lakini mkiwa mmeendelea kupitia kwa Roho Mtakatifu, mnakuwa wana na binti.

168 Sasa, wana na binti, ni nani aliye na nguvu zaidi mbele za Mungu? Malaika ni nini? Malaika ni mtumishi. Hiyo ni kweli? Wao ni watumishi Wake. Wewe ni nini? Mwana na binti Yake. Ni nani aliye na nguvu zaidi Mbinguni, basi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, au Malaika Mkuu anayesimama upande Wake wa kuume? Mwenye dhambi, ambaye ameokolewa kwa neema, ana mamlaka zaidi Mbinguni kuliko Malaika Mkuu aliyesimama kando Yake, bila dhambi, kwa sababu yeye ni mwana. Mwana ana mamlaka zaidi kuliko mtumishi, hakika.

Loo, tunasahau kile tulicho. Tunasahau, mara nyingi, kilichotufanya kile tulicho. Baada ya kuwa kile tulicho, basi tulisahau jinsi tulivyofika hapa. "Wakati Mungu Mwenyewe..."

> Loo, ni upendo wa thamani jinsi gani ambao Baba
> Aliipa jamii ya Adamu iliyoanguka;
> Akatoa Mwanawe wa pekee kuteseka
> Na kutukomboa kwa neema Yake.

Lo, jinsi tunavyopata kujua!

> Huku miamba ikipasuka na anga zikiingia giza,
> Mwokozi Wangu anainamisha kichwa chake na kufa;
> Pazia lililofunguka liliifunua njia
> Ya kuenda kwenye furaha ya Mbinguni na siku isiyo na mwisho.
>
> Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara, nasimama;
> Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.
>
> Ninapoukagua msalaba wa ajabu
> Ambapo Mfalme wa Utukufu alikufia,
> Ninahesabu dhambi yangu yote kuwa hasara tupu.

169 Hiyo ni kweli. Mmoja alisema:

Alipoishi, alinipenda; alipokufa, aliniokoa;
Alipozikwa, aliziondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, alinihesabia haki bure milele:
Siku moja Yeye yuaja—loo, siku tukufu!

170 Umekuwa ndio wimbo wa Kanisa. Umekuwa ndio mtazamo Wake. Umekuwa ndio moyo Wake. Dunia hii imeoshwa na Damu ya Mkombozi huyu wa Jamaa, kuikomboa jamii ya Adamu iliyoanguka.

171 Angalieni, Huyu hapa, Mkombozi wa Jamaa. Sasa, jambo la kwanza, ilibidi awe mtu anayestahili. Ni nani aliyestahili zaidi ya Kristo, zaidi ya Yesu? Halafu, jambo lingine, ilibidi awe na pesa. Ilibidi awe na uwezo wa kufanya hivyo. Alimiliki Mbingu. Alithibitisha alizimiliki. Angeweza kuchukua mikate mitano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, wakaokota vikapu vitano vilivyojaa vipande, baadaye. Angeweza kuvuta maji kwa pampu kutoka kwenye kisima na kuyabadilisha yakawa divai. Angeweza kumtoa samaki kutoka baharini, na kutoa sarafu kinywani mwake, za dhahabu. Amina. Yeye hakuwa ninii . . .

172 Lakini Yeye akawa maskini, hana mahali pa kulaza kichwa Chake. Akawa wa Jamaa. Sio Jamaa ya matajiri; Jamaa kwa watu wote. Alichukua mahali pa mkombozi.

173 Basi ilibidi afanye nini? Ndipo ilibidi atoe ushuhuda hadharani. Kesho yake asubuhi, Ruthu alisema, au, Naomi alisema, "Tulia, Ruthu, kila kitu kitakuwa sawa sasa, kwa sababu umepata neema machoni pake."

174 Mungu, jalia nifanye hivyo. Jalia nipate neema machoni Pake. Ndipo kutakapopambazuka:

Baragumu Yake Bwana wakati ikipigwa, na hapatakuwapo na wakati tena,
Na asubuhi ipambazuke, Milele, angavu na nzuri;
Na wakati waliookolewa duniani watakapokusanyika kwenye ule Ufuko mwingine,
Majina yaitwapo huko ng'ambo, nitakuwapo.

175 Tunatulia sasa, tukingojea ukombozi mkamilifu. Angalieni, ninayo, a—arabuni Yake, sasa. "Nilipeleka nyumbani skafu nzima iliyojaa shayiri. Nilifika huko." Akampa, akaipima, vipimo sita. Sita, ilimaanisha, "miaka elfu sita ya kuwepo kwa ulimwengu." Siku ya mwanadamu ni sita. Mwanadamu aliumbwa siku ya sita. Kutakuwa na miaka elfu sita ambayo ulimwengu uliumbwa, elfu ya saba Mungu alipumzika. Miaka elfu sita Kanisa litapambana na dhambi, kwa Nguvu za Mungu za mikate hii ya shayiri, halafu liende kwenye Raha ya Milele. Kweli. Raha, subiri. Akaweka vipimo sita vya

shayiri safi, kumdumisha hata wakati wa ukombozi mkamilifu. Ninashukuru sana kuufurahia.

176 Sasa, upesi, hebu tufike mwisho wake. Sasa tunaona, sasa, ya kwamba, kesho yake asubuhi, alipoamka, alikuwa na furaha, akingojea. Na yule mtu akaja. Akashuka. Alikuwa na jamaa mwingine ambaye kweli alikuwa na haki juu ya mwanamke huyo, kwanza. Je, nina muda wa kupata hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, hebu kidogo, nasi tutapata sehemu yake, kwa vyovyote vile.

177 Yule wa pili katika huo mfano, ambaye alikuwa na nafasi juu yako, alikuwa ni ibilisi, maana ulikuwa umetenda dhambi. Na kwanza ulikuwa wake, maana, ulikuwa, wewe ni mali yake. "Kwa maana ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uwongo." Naye hangeweza kuikomboa. Unaona? Hakuweza kuikomboa. Kwa hiyo, Kristo alikuja na akafanyika mwanadamu, kuchukua dhambi zetu, kutukomboa. Mnaliona? Wala mtu huyo mwingine asingeweza kufanya hivyo. Ibilisi asingeweza kufa kwa ajili ya dhambi, kwa sababu alikuwa ndiye mpotoshaji mwenyewe aliyefanya dhambi. Mnaona? Asingeweza. Angeharibu urithi wake, yule mtu mwingine. Naye Shetani angeuharibu wake, kwa sababu yeye ni ibilisi. Asingeweza kuwa ibilisi mwingine, kumwondoa ibilisi, ibilisi wa kwanza. Hangeweza kuwa dhambi, maana tayari alikuwa dhambi. Lakini, Kristo, akiwa hana dhambi, alifanyika mwenye dhambi. Angeweza kutukomboa. Haleluya! Tumekombolewa. *Tumekombolewa*, maana yake, "kurudishwa." Tumekombolewa.

178 Kwa hivyo, kesho yake asubuhi, basi ilimbidi kutoa ushuhuda hadharani. Alishuka akakutana na mtu huyu langoni, mbele ya wazee. Na ilibidi pawe mahali pa hadhara. Akamkazia macho. Akasema, "Je, unaweza kumkomboa?" Sasa, ilimbidi amkomboe Naomi kwanza, ili ampate Ruthu; Naye Kristo ilimbidi alikomboe kanisa la Kiyahudi, kwanza, kusudi ampate Bibi-arusi wa Mataifa. Yeye alikuja pamoja na Naomi, kama mgeni kutoka nchi nyingine, Mmoabu, wapagani. Ndivyo tulivyokuwa, Mataifa, mpagani. Basi kumbukeni, ilimbidi—ilimbidi kumpata Naomi. Basi alipompata Naomi, alipata yote aliyokuwa nayo.

179 Kumbukeni, wakati Kristo alipokuja, Yeye kamwe hakunena juu ya Kanisa la Mataifa. Ilikuwa, alienda kwa walio Wake, "Alikuja kwa walio Wake. Walio Wake hawakumpokea." Daima alikuwa kwa walio Wake. "Msiende kwa njia ya Mataifa. Msiende Samaria, bali nendeni hasa kwa kondoo wa Israeli waliopotea. Na mnapoenda, hubirini Injili, waponyeni wagonjwa, wafufueni wafu, watoeni pepo. Mmepokea bure, toeni bure." Hiyo ni kweli? Akawatuma, wawili wawili. Nendeni kwanza . . . Basi ilimbidi kulikomboa kanisa hilo. Ndipo alipolikomboa kanisa hilo, akampata Bibi-arusi wa Mataifa.

Amina. Hayo yalikuwa ndiyo maafikiano yake. Unaona? Alipata Bibi-arusi alipokomboa kanisa.

180 Sasa, Boazi, ilimbidi kufanya hadharani . . . Alisema, “Je, unaweza kumkomboa?”

Akasema, “La.”

181 Halafu ilibidi atoe ushuhuda wa hadharani. Alivua kiatu chake, akamtupia. Kasema, “Haya basi. Israeli wote na wajue kwamba nimemkomboa Naomi, na pia nimemchukua Ruthu.” Amina. “Ninamchukua Ruthu kuwa bibi-arusi wangu.” Alikuwa ni nani huyo? Bwana wa mavuno. Amina. Huyo hapo. “Ninamkomboa Naomi, kisha namchukua Ruthu. Naye Ruthu atakuwa bibi-arusi wangu.”

182 Wangesema nini? “Na awe kama—kama Lea na Raheli na hao wengine, aongeze maelfu,” naye amefanya hivyo, hiyo ni kweli, “kwa Israeli. Na awe hivyo.” Basi, angalieni, alifanya jaribio, ushuhuda wa hadharani.

183 Je, Yesu alifanya nini, apate kufanya hivyo? Alitoa ushuhuda hadharani. Wakati, Shetani hangeweza kufa kwa ajili ya dhambi kwa sababu alikuwa ndiye mwenye dhambi. Yeye ndiye baba wa dhambi. Ila, Yesu, Yeye asiye na hatia, Mungu wa Mbinguni, ambaye haikumbidi kufa, alishuka akatoa ushuhuda wa hadharani kwa kufa, akainuliwa kati ya mbingu na nchi. Ushuhuda wa hadharani; akavuliwa nguo Zake, na kuning’inia kati ya mbingu na nchi, katika aibu. Kisha akafa, kifo cha dhambi, cha aibu, apate kutukomboa. Ushuhuda wa hadharani! Amina.

184 Alifanya nini? Akaondolea mbali haki Yake mwenyewe; akaondolea mbali utukufu Wake. Akaondolea . . . “Ninazo nguvu. Ningenena na Baba Yangu, na mara moja angenitumia vikosi ishirini vya Malaika.” Wangeweza kuubadilisha mwelekeo. Malaika mmoja angeweza kufanya hivyo. Angeweza kuagiza vikosi ishirini. Hiyo ingekuwa kama Malaika elfu arobaini. Wangeweza kufanya nini? Alisema, “Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu, mara moja, hiyo ni sasa hivi, Yeye angenitumia vikosi ishirini. Vikosi vya Malaika watakuja hapa na kuiteka hii.” Mmoja angefanya nini? Mmoja angeiangamiza dunia, katika sekunde moja. Angalieni tu, Yeye alikuwa na maelfu wangelikuja. Mnaona? Lakini aliliondolea hilo mbali. Akaweka hilo kando. Aliweka hadhi Yake yote, kila kitu, kando, akawa mwenye dhambi na akafa kwa ajili yako na yangu.

185 Sasa, katika kufunga, huenda tukasema hivi, katika kufunga. Alifanya—alifanya hivyo. Kisha akamchukua Ruthu, akamwoa. Akazaa mtoto wa kiume aliyeitwa Obedi. Obed alikuwa baba wa Yese. Yese alikuwa baba wa Daudi, ambaye alikuwa baba wa Kristo, amina, baba wa Bwana Yesu.

186 Huoni? Kupitia haki hiyo, kupitia uamuzi huo dhahiri, Yeye alifanyika Mkombozi wetu wa Jamaa. Mungu akawa wa mbari

yetu, kushuka na kufanyika kama sisi, mwanadamu, kuona njaa, kuona kiu. “Naona kiu. Nipe maji ninywe.” Nao wakatia siki kinywani mwake, nyongo. Aliona kiu kama sisi. Alijua jinsi ya kuenda bila.

187 Alikuwa mgonjwa kama sisi. Alisema, “Je, si wataniambia methali ya kale, ‘Tabibu, jiponye nafsi yako’?” Lakini nguvu zake kuu hazikuwa kwa ajili Yake. Alikuwa na nguvu za kufanya hivyo, lakini asingeweza kuzitumia kwa nafsi Yake. La.

188 Mtu fulani aliniambia, hivi majuzi, akasema, “Ndugu Branham, kabla ya jambo lolote kutokea, unajua yote yatakayokupata.”

189 Nikasema, “Hii karama si kwa ajili yangu. Siwezi kuitumia kwa nafsi yangu.” Ni kwa ajili yenu. Ninyi ndio mnaopata faida, sio mimi. Mimi ni mtumishi wa umma wa Mungu tu, kwenu.

190 Mhubiri ni mtumishi wa umma. Anajishikilia tu hapo. Kama vile yungiyungi ya kondeni, nyukibambi huruka ndani, anapata sehemu yake. Nyuki wa asali anaruka na kupata yake. Mpita njia anapata yake, na kila kitu. Hilo hufanya kazi kwa bidii, usiku na mchana, lipate kuendelea kunawiri. Naye mhudumu wa Injili hufanya jambo lile lile; hutembea katika mstari wa Mungu. Anashikilia ushuhuda wake vema, ulimwengu upate kumshiriki, unaona, Bw. Mchungaji Yungiyungi. Yeye ni mzuri. Yesu alisema, “Mtafakarini. Sulemani si kama yeye.” Hiyo ni kweli. Dk. Yungiyungi, nadhani nyote mnamfahamu. Mnaona?

191 “Yatafakarini maua ya kondeni, jinsi yanavyotenda kazi na kusokota, wala. Nasema, na, hata hivyo, Sulemani, katika fahari yake yote . . . ” Yungiyungi halina budi kujitahidi, mchana na usiku, lipate kunawiri lihifadhi mavazi yake, kuyaendeleza manukato na kadhalika. Na wengine . . . Yeye hujifunua tu mwenyewe, na wanakuja na kuyatoa kwake. Nyuki na nzi, na kila kitu, huja hapo, wema au wabaya, huchukua tu kutoka kwake.

192 Ndivyo alivyo mtumishi, wa Kristo, Mkristo mtumishi; hujifungua mwenyewe, “Chukueni tu kutoka kwangu, walimwengu.” Hakuna kitu kwa ajili yake mwenyewe. Ni kwa ajili ya wengine. Hicho ndicho Kristo alifanyika wakati alipofanyika jamaa kwetu. Alifanyika mtu, ulimwengu upate kushiriki haki Yake, unaona, na kufanywa wana wa Mungu.

193 Sasa, walifanya nini? Walifunga ndoa, na kupitia hiyo likaja jambo hili kubwa. Ndipo Ruthu akapewa thawabu, kwa kumpata Kristo . . . au kumpata Boazi kama mumewe. Ambapo, Kanisa limepewa thawabu, hapo Kuja kwa Bwana kutakapotukia, katika asubuhi hiyo angavu na isiyo na mawingu. Tunapumzika, tukisubiri sasa. Itakuja. Sasa, kwa nini? Imekombolewa.

194 Sasa, nukuu moja zaidi kabla sijaondoka, kuanzisha mstari wa maombi. Nukuu moja zaidi. Nililichunguza, asubuhi ya

leo, neno *komboa*. Nilininii tu. . . Samahani, ndugu zangu wa Kiarminia, bali sina budi kuingiza hili; sio kudhuru, ila tu kuwafanya muwazie. Chunguzeni kile *ukombozi* unachomaanisha. Ukombozi, kwa kweli unatumika, katika neno la Kiyunani, kumchukua mtumwa kutoka sokoni. Siwezi kutaja herufi za hilo neno la Kiyunani sasa, bali linamaanisha, "kumchukua mtumwa kutoka sokoni," *kukomboa*.

195 Mtu amefanya jambo baya, kwa hiyo, yeye, bwana wake alimuuza utumwani, haswa hata kifo. Naye yuko sokoni, yeye ni mtumwa. Lakini mtu anakuja, mtu mstahilifu anayeweza kufanya hivyo, ndipo anamwona mtu huyu, naye anapata kibali machoni pake, anamkomboa. Hiyo ni kumwondoa kutoka kwenye soko la watumwa, anampeleka nje kwake mwenyewe. Angalieni. Na mtumwa huyo, akisha kukombolewa, hawezi kuuzwa sokoni tena. Amina. Hawezi kuuzwa tena. Ametiwa alama. Na ikiwa alifikiriwa vya kutosha, wakati mmoja, kukombolewa, hakuna mtu anayeweza, kamwe, kumuuza tena kama mtumwa.

196 Loo, ashukuriwe Mungu, kwamba wakati mtu amekuja kwa Kristo mara moja na kukombolewa na Damu ya thamani, ibilisi hawezi kukufanya mtumwa tena. Uko salama katika Damu ya Yesu Kristo hata siku ya ukombozi wako. Mtumwa, itafute katika Kutoka, uone kama hizo sio sheria za Walawi. Namaanisha, katika Mambo ya Walawi, uone kama hiyo siyo sheria. Mtumwa, akiisha kukombolewa, hawezi kuuzwa tena kama mtumwa. Hiyo ni kweli.

197 Loo, nina furaha sana! Nina furaha sana kujua kwamba Mkombozi wetu wa Jamaa, kwamba Mungu wa Mbinguni, Yule aliyekuwa Roho, alishuka duniani na kufanyika mwili; akafanyika jinsi nilivyo mimi, akafanyika kama ulivyo wewe; kisha akachukua umbo la mwili wenye dhambi, bila kujua dhambi, ili dhambi zetu ziwe juu Yake; na kuwa jamaa yetu, alifanya ushuhuda wa hadharani wa kufa, kulipa gharama kamili.

198 Naye Roho wa Mungu anashuhudia tena. Hekalu likapasuka, lile pazia, kutoka juu hadi chini. Sio kutoka chini hadi juu, bali kutoka juu hadi chini; ikaonyesha ya kwamba ilikuwa ni Mungu, Mwenyewe, aliyeirarua, kutoka Juu. Akairarua kutoka juu hadi chini, na kuifungua njia. Ndipo bloku za dhabihu zikapinduliwa, na radi ikamulika kwa ndimi zake gizani, anga zenye hasira. Jua likatua katikati ya mchana. Nyota zilikataa kuangaza. Na kila kitu kikatoa ushuhuda, "Tumekombolewa." Haleluya!

Na tuombe. [Ndugu fulani anatoa matamshi ya kinabii—Mh.]

199 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, hebu kidogo. Hayo yalikuwa matamshi ya kinabii, yakiliita kanisa, baada ya Ujumbe.

200 Sasa ikiwa kuna wengine hapa wasiomjua, maisha yenu sio sawa, mmealikwa sasa kusimama hapa mbele ya kusanyiko hili, uso wa Mungu, kumkubali kama Mwokozi wako. Maji yamo kwenye kidimbwi kwa ajili ya ubatizo. Ikiwa mtu anasubiri kuanza ibada ya ubatizo, mara moja.

201 Wakati tumeinamisha vichwa vyetu, tutachukua wakati huu sasa kwa kuimba *Ninapitia*, huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa.

> Ninapitia, naam, ninapitia,
> Nitalipa gharama, haidhuru wengine wanafanya nini;
> Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa;
> Nimeanza na Yesu, nami ninapitia.
>
> Ninapitia, naam, ninapitia.
> Mimi . . .

Kweli unalimaanisha sasa? Kama ndivyo, njoo hapa na usimame.

> . . . haidhuru wengine wanafanya nini;
> Nitachukua njia . . .

Je, uko tayari kushikilia?

> . . . ya Bwana . . .

Kama Naomi wa kale?

> Nimeanza pamoja na Yesu, nami ninapita.
>
> Kutoka hori la Bethlehemu alikuja Mgeni,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,
> Naomba tu kuwa kama Yeye.
>
> Kuwa kama Yesu, . . .

Unataka kuwa kama Mkombozi wako?

> . . . kama Yesu,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,
> Naomba tu kuwa kama Yeye.
>
> Niangazie, Bwana, niangazie,
> Nuru kutoka Nyumba ya taa iniangazie;
> Niangazie, Bwana, niangazie,
> Jalia Nuru kutoka Nyumba ya taa iniangazie.
>
> Kuwa kama . . .

Kulikuwa na mtu mwingine yeyote ambaye ungependa kuwa kama yeye, zaidi ya Yeye? Hivi mtu mwingine hatakuja sasa na kupiga magoti hapa pamoja na msichana huyu, anapopiga

magoti? Kushika, kama Ruthu wa kale, kushika njia yake asubuhi ya leo.

. . . kama Yeye;
Kote katika . . . duniani hata Utukufuni,
Naomba tu kuwa kama Yeye.

Kuwa tu kama Yeye . . .

Mtu mwingine aje sasa. Atembee hapa chini na kupiga magoti, kama mama huyu alivyofanya hapa. Umeanza? Je, utaweka mikono yako katika Yake?

. . . Natamani kuwa kama Yeye;
Kote katika safari ya maisha kutoka duniani
 mpaka Utukufuni,
Naomba tu kuwa kama Yeye.

[Ndugu Branham anavumisha *Kuwa Kama Yeye*—Mh.]

202 Baba yetu wa Mbinguni, wakati kanisa linapouvumisha wimbo huu, "kuwa kama Yesu," mwanamke huyu, asubuhi ya leo, ametoka nje, kama Ruthu. Ina Bell, akija kama Ruthu wa zamani. Haijalishi gharama ni nini, amekuja kuilipa. Haijalishi nini . . . jinsi atakavyochekwa, au kudhihakiwa, anachukua nafasi sasa, akisimama hapa, akikiri dhambi zake. Akipiga magoti, akiangalia mahali ambapo Bwana mkubwa wa mavuno alilala msalabani. Na pale kupokea Roho Wake, neema Yake iliyosema naye wakati Neno lilipokuwa likitoka, kama Naomi wa kale, akielekeza. Nayo ilimgusa anayefaa, mahali sahihi. Na sasa anakuja kuchukua nafasi ya mwaminio, amepiga magoti pale msalabani, hapo ambapo anakiri dhambi zake, anaweka kando mambo yote ya zamani ya maisha, na kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

203 Tunaomba, Baba, asubuhi ya leo, kwamba kila mtu aliyetengwa katika jengo hili, kila mwanamume, mwanamke, mvulana, au msichana, asiyekujua Wewe, usiruhusu Maneno haya yapite, Bwana. Hatujui ni saa gani tutakayoingia Hukumuni. Bado ingali inawezekana kwamba leo hii ndiyo wengi wetu huenda ikatulazimu kuja. Labda kabla ya kufika nyumbani, ajali itatokea. Huenda . . . Ugonjwa wa moyo unaweza kutushika. Hatujui. Ee Mungu, jalia tujitenge, saa hii, wakati Roho akiwa hapa, wakati tukiwa na ushahidi kwamba yuko hapa, wakati Mungu wa Mbinguni, katika rehema Zake zote zisizo na kipimo, akiwa hapa kutuingiza ndani.

204 Tupe neema Yako, Bwana. Tuma wengine, asubuhi ya leo, madhabahuni, na wampokee Kristo kama Mwokozi, kama anavyofanya mwanamke huyu sasa. Lijalie, Bwana. Mrehemu, ukijua kwamba watu wake . . . Ndugu yake ameketi hapa jukwaami pamoja nami. Dada yake, Wood, akiketi pale nje; mama na baba wamekaa hapa. Bwana Mungu, naomba rehema. Lijalie, Bwana. Unajua ninachomaanisha moyoni mwangu. Ninaomba kwamba kumwaga kwako Damu yako, katika

rehema, kutakuja sasa kwenye saa hii. Tujalie, Bwana. Tujalie, tunapowangojea wengine, jalia wengine waje, pia, Baba, na wapatanishwe na Mungu kupitia Kristo.

205 Na sasa, wakati tukingojea sasa na kushangaa, tutaimba tena.

> Niangazie, Ee Bwana, niangazie.
> Jalia hiyo Nuru kutoka kwa Mnara wa taa iniangazie.

Sawa. Naam.

> Angaza . . .

Kunaweza kuwa na mwingine?

> . . . iniangazie,
> Jalia Nuru kutoka Mnara wa taa iniangazie;
> Niangazie, Bwana, niangazie,
> Jalia Nuru Yako kutoka kwa Mnara wa taa, iangaze . . .

Itanifanyia nini?

> Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maisha kutoka duniani mpaka Utukufuni,
> Naomba tu kuwa kama Yeye.

206 Baba Mungu, huo kweli ndio ushuhuda wetu. Bwana, tunataka kufanana na Yeye, wapole na wanyenyekevu, waliojitweza, watamu, daima akiwasamehe wale wanaomtendea vibaya na kufanya vibaya. Sisi—sisi tunataka kuwa hivyo. Tunakushukuru kwa ajili ya mwanamke huyu aliyekuja asubuhi ya leo. Tunajuaje maisha haya yatakuwa nini, baada ya muda mfupi? Labda kupitia makosa yake yote na vitu maishani, kama vile sisi sote tumefanya, kuyaona yametumbukizwa chini ya mafuriko asubuhi ya leo. Ninaomba, Mungu, kwamba mwanamke huyu ataishi maisha yaliyowekwa wakfu yatakayowaongoza wenzake wote kwenye ujuzi huu. Jalia asikomee hapa, bali aende aingie katika nchi ya ahadi, akipaangalia mahali hapo na kujilaza chini, ampokee Roho Mtakatifu hapo. Tujalie, Bwana.

207 Kama kukiweko na wengine zaidi humu ndani, Baba, ambao walipaswa kuja, wala hawakuja, jalia Roho Wako asiwaache. Jalia wasipate raha, usiku wala mchana, mpaka watakapokuja, pia, wafanye uamuzi uu huu. Sio kuwa mkali, Bwana, lakini, Ee Mungu, nikijua wanachokosa. Kujua itakavyokuwa kwenye Siku ile, kumsikia Yeye akisema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Asubuhi hiyo, katika Mtaa wa Nane na Penn, nilikuita, wala hukuja." Ee Mungu, hiyo itakuwa ni saa ya kutisha jinsi gani kwao, tutakapopimwa kwenye mizani na kupatikana tumepungukiwa. Baba, jalia kwamba hiyo haitamjia mtu

yeyote aliye katika Uwepo wa Kiungu. Jalia wote waokolewe. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

208 Tunataka kumshukuru Bwana, asubuhi ya leo, kwa ajili ya wema Wake na fadhili. Ninawashukuru nyote kwa uvumilivu wenu, wa kungojea pamoja nami muda mrefu hivi.

Dada Ina Bell. Mimi . . . Dada Wood, huyo ni dada yako, Ndugu Charlie. Kile wamekuwa wakiombea, na kile tumeombea, kwa muda mrefu. Dada Ina Bell, unaweza kusimama, kwa muda kidogo tu? Huyo ni wa Dada Wood . . . Mdhamini wetu hapa kanisani, huyo ni shemeji yake, ambaye amemkubali Yesu kama Mwokozi wake binafsi asubuhi ya leo. Na ni sala ngapi zimekuwa . . . Mungu akubariki, Dada Ina Bell. Nadhani nimelitaja jina lako sawa. Hiyo ni kweli? Mungu na aendelee kukubariki, dada mpendwa. Na ikiwa hujawahi kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, nakusihi ufanye hivyo, na umpokee Roho Mtakatifu.

209 Mungu daima awe pamoja nawe, ambariki mume wako wa thamani huko. Nilikutana naye, siku chache zilizopita. Ikiwa sijakosea, jina lake ni Stanley. Hiyo ni kweli? Stanley. Mungu akubariki, Stanley. Nyumbani ni kutamu, lakini naamini kutakuwa kutamu zaidi kuliko hapo awali. Mungu daima awe pamoja nanyi nyote, na—na kuwapa neema na rehema Zake, siku zote za maisha yenu. Basi mfuate Bwana. Kuwa kama Ruthu sasa, Ina Bell, shikilia Kwake. Endelea tu kusonga mbele. Wakati mwingine itakuwa ngumu, na njia zitaingia giza kidogo. Lakini, kumbuka, angalia chini tu kuelekea ardhini, kisha angalia juu kuelekea angani, utapata nyayo za Damu ambazo zinafuatisha moja kwa moja hadi huko juu. Atakuwa akiongoza njia.

210 Sasa, loo, tayari ni adhuhuri, saa sita. Mngali tayari kufanya mstari wa maombi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

211 Billy, wapi, ni aina gani . . . ? Je, alisambaza kadi za maombi? Mimi—mimi kamwe . . . Ninaamini aliniambia alisambaza maombi . . . Vema, ilikuwa nini? Mtu fulani aniambie herufi na namba zilikuwa zipi. [Ndugu mmoja anasema, "Huyo hapo anakuja."—Mh.] Nini? [Ndugu Billy Paul anasema, "B."] B. B, moja hadi mia moja? Hamsini hadi mia moja. Sawa. B, namba moja. Walipata . . .

212 Sasa, tuna umati wa watu, kwa hivyo hatuwezi . . . Tutawafanya wote wasimame, nasi tutawapitisha tu, wakati nikiwaombea.

213 Sasa, ni wangapi hawajawahi kuona moja ya mistari ya maombi? Hebu tuone mikono yenu, hujawahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu, kwenye mstari wa maombi. Loo, jamani! Wengi wenu.

214 Kweli, sasa, tunaweza tu kuwaombea watu, au tunaweza kuwa na upambanuzi, au tusiwe na mstari wowote wa maombi; tuwaite tu, katika kusanyiko. Haijalishi. Roho Mtakatifu yuko

hapa. Naam, bwana. Lakini hebu tuwe tumesimama kwenye mstari wa maombi.

Namba moja, ni nani aliye na namba moja, kadi ya maombi B? Nam-. . . Hamsini. Samahani. Hakuna aliye na moja, kusema kweli. Vema. Kadi ya maombi hamsini, ni nani aliye nayo? Njoo hapa, bwana. Kadi ya maombi mbili . . .

Hamsini na moja, hamsini na mbili. Kadi ya maombi hamsini na mbili. Vema. Hamsini na tatu. Hamsini na tatu. Vema. Hamsini na nne.

Njoni huku, papa *hapa*. Ikiwa uko huko nyuma, njoo huku, *hapa*.

Hamsini na moja, hamsini na mbili, hamsini na tatu, hamsini na nne. Ni nani aliye na hamsini na tano, kadi ya maombi hamsini na tano? Mama huyu, papa *hapa*. Kadi ya maombi hamsini na sita.

Simama, kando ya ukuta, *pale*, tafadhali.

Hamsini na saba, hamsini na nane, hamsini na tisa, sitini. Sitini na moja, sitini na mbili, sitini na tatu, sitini na nne, sitini na tano.

Busty, pita kulia kupitia kwenye marefu hayo papo hapo, ndugu, papo *hapo*. Vema. Geuka moja kwa moja.

Ni wangapi hawana kadi ya maombi, nawe unataka Bwana akuponye? Inua mkono wako. Vema. Hivyo ndivyo tu ikupasavyo kufanya, amini hilo tu sasa. Amini tu. Vema.

Hamsini na sita. Nilikuwa nayo? Hamsini na saba, hamsini na nane, hamsini na tisa, sitini. Hebu wasimame.

Sitini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano. Hebu wasimame. Sitini na sita, sitini na saba, sitini na nane, sitini na tisa, sabini. Hebu wasimame.

Sitaki wote wakimbie kwa wakati mmoja, ndiyo sababu ninaita hizo namba, hadi sabini.

Sabini hadi themanini, simameni. Njoni hapa, upande *huu*, sabini hadi themanini. Vema. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa. Vema.

Themanini hadi tisini, simameni *hapa*. Doc, wasaidie huko nyuma, tafadhali. Themanini hadi tisini, simameni upande *huu*.

Tisini hadi mia moja, simameni upande huu, *hapa*. Vema.

215 Wakati wakijipanga, ningependa kuuliza kanisa jambo fulani. Ni wageni wangapi walio hapa, hawajapata kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo awali? Ni wangapi wenu? Ni wangapi wanajua kwamba hakuna mtu anayeweza kumponya mwingine, si hata daktari? La, bwana. Daktari si mponyaji. Yeye husaidia tu maumbile. Mungu ndiye mponyaji. Unaona? Daktari anaweza kuunganisha mkono, lakini hawezi kuuponya mkono. Daktari anaweza kuondoa kidole tumbo, lakini sio kuponya

mahali alipokata. Daktari anaweza kung'oa jino, lakini sio kuzuia kutokwa na damu, wala kupaponya. Mungu hana budi kufanya hivyo. Vema.

216 Ni wangapi wanajua kwamba, wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, kwamba Yeye hakudai kuwa mponyaji? Alikuwa Mwanadamu. Alisema, "Sio Mimi nizitendaye hizo kazi, bali Baba Yangu aishiye ndani Yangu, Yeye hufanya hizo kazi." Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua, wakati alipokuwa hapa, nini, jinsi gani . . . Alikuwa na huduma ya aina gani wakati alipokuwa hapa? Alifanya kile Baba alichomwonyesha kufanya. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Ni wangapi wanajua, wanajua hilo? Yohana Mtakatifu 5:19, Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya neno Mwenyewe, bali kile anachomwona Baba akifanya." Hiyo ni kweli? ["Amina."] "Ndivyo afanyavyo Mwana, vivyo hivyo."

217 Sasa, basi, je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaamini hivyo, kwa moyo wako wote? ["Amina."] Yeye ni yule yule jana na hata milele. Unaamini, kwamba, Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele, kwamba hiyo inamaanisha Yeye kweli ni yeye yule? ["Amina."] Sawa.

218 Yeye ni yule yule vipi? Yule yule katika kila kanuni. Hiyo ni kweli? Yeye ni Mungu yule yule, Mponyaji yeye yule—Mwokozi yeye yule. Yeye ni yeye yule, mtazamo ule ule. Hiyo ni sawa. Hiyo ni kweli? Sawa. Sawa. Halafu, ikiwa alikuwa yule yule, na ni yule yule, atafanya na kutenda sawa. Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wanajua hiyo ni Kweli?

219 Nitachukua dakika moja tu hapa. Nasubiri. Haionekani, kwangu mimi, kana kwamba hao ni watu hamsini wanaosimama hapo. (Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne.) Hapana. Baadhi yao labda walikwenda nyumbani, mapema. Niliwaona watu wengine wakiondoka kule nyuma. Sawa, hii kidogo tu, laini fupi. Ni wangapi wangependa kuwa na hii? Ni wageni wangapi kwangu, kwenye mstari huo? Inua mkono wako, unayejua sijui chochote juu yako. Inua ninii wangu . . . mkono wako.

220 Ni wangapi huko nje, wageni, wanaojua sijui chochote juu yenu? Inua mkono wako, kwamba wewe ni mgonjwa. Vema. Ni wangapi wangependa kuona mstari wa upambanuzi, ili tupate kuharakisha tu na kumalizia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mngependa . . . ? Sasa, haijalishi. Ninaweza kuwaombea tu, niwapitishe moja kwa moja mstarini. Au, wanaweza kukaa chini, waende tu waketi. Haijalishi. Roho Mtakatifu anaweza kuitambua, vile vile tu. Unaamini hivyo?

221 Sasa, basi, ikiwa ni hivyo, basi nyamazeni tu, kwa muda mfupi tu. Tunachelewa kidogo, kwa hivyo kaeni kimya tu, kwa muda mfupi tu. Nataka kuwaulizeni jambo fulani sasa.

222 Ninaweza kuwa kwenye maikrofoni mbaya hapa. Zote mbili ni sawa? Zote zimeunganishwa, vema, *hii* pia? [Ndugu anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sawa.

223 Sasa, kaeni kimya tu, kwa muda mfupi. Nitaangalia chini kwenye mstari huu, nione kama ninamfahamu mtu yeyote.

224 Namjua jamaa huyo anayesimama papo *hapo*. Sasa, namjua Earl. Earl, nakujua, Earl Colvin. [Ndugu Earl Colvin anasema, "Siko kwenye mstari wa maombi, hata hivyo, Ndugu Bill. Nilimleta rafiki yetu kutoka Jeffersontown."—Mh.] Loo, ndiyo, naam, mtu huyu hapa juu. Huyo ndiye yule mtu tuliyewinda naye, kule juu Colorado? ["Labda hutatutambua, tumepoteza uzito mwingi sana."] Loo, jamani! Hakika siwatambui. Ninaamini Earl aliniambia kuwa ulikuwa mgonjwa sana, na umekuja. Sasa, ikiwa huwezi kusimama kwa muda mrefu, hebu mtu ampelekee kiti hapo. Ama, baadhi yao—baadhi yao wasimame na kumpa kiti hapo karibu, itakuwa ni sawa, maana huyo mtu ni mgonjwa sana, sana. Jamani! Amepoteza karibu pauni mia moja au zaidi, ya uzani. Na—naye—yeye ni mgonjwa sana, sana. Sasa acha aketi tu hapo. Anza kumshukuru Yeye, hapo, ndugu.

225 Sasa hebu niangalie chini. Sasa, Earl alikuwa amesimama tu pamoja naye. Sasa, mtu *huyu*, anayesimama pale nyuma, akiniangalia, kutoka kule karibu na La—LaGrange, Kentucky. Sijui jina lake, lakini na—na—nakujua. Na huyo ni Ndugu na Dada Kidd hapo. Ninawajua. Na mwanamke huyu, sawa. . . Je, huyo ni Dada Rook? Au. . . [Ndugu Neville anasema, "Dada Hardy." Dada mmoja anasema, "Mimi ni Dada Taylor. . .?. . . pamoja na Hattie."—Mh.] Pamoja na mwanamke huyu hapa, kutoka Sellersburg, ninaamini, ambaye ni kipofu. Hiyo ni kweli? Vema.

226 Nafikiri hao ni karibu wote, mstarini, ambao kweli nawajua. Loo, naam, huyu hapa rafiki yangu msiri, Busty Rogers, hapa, kutoka huko chini Milltown. Na chini kwenye mstari, nadhani wengine wote hatufahamiani. Sasa, hiyo ni mbele za Mungu, nijuavyo mimi, hatufahamiani.

227 Sasa hebu nione kwenye kusanyiko. Sasa, ninyi—ninyi ambao hatufahamiani, ambao ni wagonjwa, inua mkono wako, na, unajua, una haja moyoni mwako. Inua mkono wako, popote ulipo. Anayejua mimi. . . Vema. Sawa. Ni vivyo hivyo tu, kote, karibu kila mahali.

228 Sasa, sasa, haitawadhuru, kusubiri tu kwa dakika moja ama mbili zaidi. Ninataka kuwaulizeni swali zito. Ni afadhali nirudi hapa nyuma, ili muweze kunisikia. Nataka tu kuwaulizeni jambo fulani. Sasa, hizi Jumbe ninazohubiri, mnaziamini ni Kweli?

[Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wewe, hakika, usingekuja hapa kama sivyo.

229 Sasa je, Mungu angefanya kitu kama hicho bila kunipa dhana ya kile nilichokuwa nikifanya? Hakika asingefanya hivyo. Hakika, asingeweza. Sasa, ikiwa amefanya hivyo . . .

230 Sasa, ninadai kwamba Yesu Kristo hajabadilika. Kifo chake hakikumbadilisha; kilimtukuza. Naye alifufuka, siku ya tatu, akapaa Juu. Naye akamtuma tena Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa ni Mungu, ndiye Roho Mtakatifu aliyekuwa juu Yake. Nyote mnaamini hilo? Naye Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo, na *ulimwengu* hautaniona Mimi tena.” Huo ni utaratibu wa ulimwengu, mnajua, kanisa tu lisiloamini na yote. “Hawataniona Mimi tena. Hata hivyo, ninyi mtaniona Mimi.” “Nyinyi,” hilo ni Kanisa, mwaminio. “Kwa kuwa Mimi . . . ” *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. “Mimi nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Na Kiyunani hapo ni *ukamilifu*, ambalo linamaanisha, “mwisho wa ulimwengu.” “Kuwa pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu. Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Je, hiyo ni Kweli?

231 Sasa, tuna Wabaptisti, Wamethodisti, Waprotestanti, na Wakatoliki, na—na hata Myahudi, wameketi hapa asubuhi ya leo. Na tuna Church of God, Nazarayo, Pilgrim Holiness, Shahidi wa Yehova, madhehebu yote tofauti yamewakilishwa. Ninatazama kote, nikiwaangalia. Wamethodisti, Walutheri, Wapentekoste, yote mbalimbali, ninapoangalia kote, ninaona watu ninaowajua. Na wote ni wageni kutoka nje ya mji. Maskani ya Branham ni kitu kidogo sana, hapa m—mjini, lakini inaujumuisha ulimwengu.

232 Sasa, hebu tuchukue hii tu, na kuwazia kwa makini kabisa, tuwazie, tusome, tuwe na kicho, na kuuliza swali hili. Basi, ikiwa Yeye hajafa, basi mtazamo Wake kwako na kwa wagonjwa ungekuwa sawa tu leo hii kama ulivyokuwa jana. Basi alichukua msimamo Wake vipi jana? Huu, “Ninaweza, kama ukiamini.” Hiyo ni kweli? “Kama ukiamini.”

233 Yule mtu akasema, “Bwana, uturehemu.” Kasema, “Mwanangu amepagawa sana na pepo. Nilimleta kwa wanafunzi Wako, nao walikuwa wakipiga mayowe na kupaza sauti, na kila kitu.”

234 Alisema, “Ninaweza, kama ukiamini. Ukiamini, ninaweza.”

235 Sasa angalieni. Yesu alifanyaje? Alikuwa nini, jana? Alihudumuje? Sasa, hii ni kwa mgeni sasa, ndiye ninayemzungumzia. Hebu tuone kile alichokuwa, jana. Itanichukua tu kama dakika tatu, tutanukuu, sehemu kadhaa ndogondogo.

236 Wakati huduma Yake ilipoanza, kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Andrea, mvuvi, akaongoka, akamwamini, kisha akaenda akamleta ndugu yake, jina lake Simoni. Mnakumbuka hayo? Alimleta kwa Yesu. Alikuwa mvuvi asiye na elimu, hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Basi akaja mbele ya Yesu. Yesu akamwangalia, akasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona."

237 Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko? Walijua huyo alikuwa ndiye Masihi, maana Yeye ni . . . Mungu aliahidi. Musa aliahidi, kwamba, Masihi ajapo, Yeye atakuwa Nabii. Hiyo ni kweli? Nabii-Masihi. Akaangalia, akasema, "Jina lako ni Simoni." Tena akasema, "Baba yako aliitwa Yona." Ndipo akajua huyo alikuwa ndiye Masihi.

238 Yule mwanamke kisimani, hilo ni taifa jingine la watu. Sasa, ni Wayahudi tu na Wasamaria waliompokea. Mataifa, tulikuwa hatujaingia bado, kikundi cha Ruthu. Sasa, yule mwanamke kisimani, ambaye alikuwa Msamaria, alikuja kuteka maji. Yesu akasema, "Nipe maji ninywe." Alifanya nini? Alizungumza naye, kama vile tu ningezungumza na mtu huko kwenye kusanyiko. Kasema, "Nipe maji ninywe." Hawakuwahi kukutana hapo awali.

239 Naye mwanamke huyo akasema, "Mbona, sio kawaida, tuna ubaguzi hapa." Kama ilivyokuwa huko Kusini, kwa marafiki zetu weusi na kadhalika, lakini hawanao tena. Mungu ashukuriwe, kwa hilo. Basi akasema . . . "Tuna ubaguzi hapa. Mbona, sio kawaida Kwako. Wewe ni Myahudi." Yesu alikuwa Myahudi. Huyo mwanamke alikuwa ni Msamaria. Kasema, "Sio kawaida kwa—kwako Wewe kuniomba, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho."

240 Akasema, "Lakini, mwanamke, kama ungalijua ni Nani unayesema Naye, ungeniomba Mimi maji."

241 Hiyo ilimsimamisha mwanamke huyo mrembo. Naye akaangalia juu akasema, "Mbona, huna kitu cha kuchotea. Kisima ni kirefu."

242 Akasema, "Maji ninayotoa ni Uzima wa milele."

243 Basi mwishowe aligundua shida yake ilikuwa nini. Ni wangapi wanaojua, wageni, wanaojua shida yake ilikuwa nini? Alikuwa na waume watano. Kwa hivyo alimwambia nini? Alisema, "Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa."

244 Akamtazama. Akasema, "Sina mume yeyote."

245 Akasema, "Umesema vema, kwa maana umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

246 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii. Sasa, tunajua, Masihi atakapokuja," (Huyo ni Yesu.) "Masihi atakapokuja, Yeye atatuambia mambo haya, maana tunajua

Yeye atakuwa Nabii huyo. Tunajua Masihi atakapokuja, atafanya hili. Lakini U Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

247 Na juu ya hayo, alikimbilia mjini na kusema, “Njoni, mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyofanya: Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi mwenyewe?”

248 Ikiwa hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi jana, na Yeye ni yule yule leo, ni jambo lile lile leo. Sasa, je, ninyi wageni mnaamini hivyo? Sasa, hiyo ni kwa ajili yenu *hapa* mstarini.

249 Sasa, kwao walio huko nje, Andiko moja tu, ili muwe na kitu cha kusimamia. Ni wangapi wanaoamini kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu sasa, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Sote . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . .

Baba wa Mbinguni, Yule anayenijua, anayejua, nijuavyo mimi, sijawahi kumuona mtu huyo. Sasa huenda ikawa yeye ameniona na labda naweza kuwa nilimwona, lakini kama tumeonana sijui chochote juu yake. Maana, nimekuwa kote ulimwenguni, mara nyingi, nikiwaombea wagonjwa na kadhalika, na mimi—mimi huenda nimekutana naye mahali fulani, au kumwona, au chochote kile, sijui. Lakini hata hivyo, si—sijui chochote kumhusu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, bwana? Ili tu watu wajue. Mnaona? Sawa. Sasa, mtu huyo amesimama hapa kwa sababu fulani. Sasa huyo jamaa yuko wapi ambaye ni mwindaji, Efferson, au, yeyote- . . . Vema. Nataka tu alione. Yuko wapi, Busty Rogers yuko wapi? Amesimama tu pale. Sasa hapa, sasa Busty, unanijua. Bw. Efferson, unajua (Hiyo ni kweli? Efferson? Naam.), unanijua, tuliwinda pamoja huko Colorado, mimi—mimi ni mwanadamu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

250 . . . Mtu anaugua ugonjwa wa hali ya wasiwasi. Hiyo ndiyo shida yake; maana una tezi dume (Hiyo ni kweli.), kuamka usiku, na kadhalika. Unatoka Ohio. Nawe ni wa kanisa la Ndugu Sullivan au unaenda huko. Namwona Ndugu Sullivan amesimama hapa. Umekuja na akina Kidds; huyo ndiye uliyekuja naye. Hiyo ni kweli. Vema, kwenye wakati huu unajisikia tofauti sasa. Umekuacha. Sasa, unaweza kwenda nyumbani; imani yako imekuponya. Sasa, Mungu akubariki.

Sasa unaamini?

251 Sasa sikujui wewe, bwana. Inaonekana naijua sura yako, lakini sasa, kuhusu kukujua, Mungu Mbinguni anajua, sijui chochote kukuhusu. Sijui una shida gani. Nisingekuwa na njia ya kujua shida yako ni ipi. Wewe ni mtu tu anayesimama hapo. Nawe ulikuwa na kadi ya maombi, yenye . . . ilikuwa na namba juu yake. Nawe unaninii tu . . . Mvulana huyo alikupa kadi hiyo, nawe uliitwa tu hapa kwenye mstari wa maombi.

252 Sasa, angalia tu jinsi inavyoibuka. Unaona, mara hiyo moja tu, hiyo ni ngumu zaidi, hiyo imenifanyia mengi zaidi, mara hiyo

moja, kuliko wakati wote ambao nimekuwa nikihubiri asubuhi ya leo. Kitu fulani kikitoka. Mnaona? Kitu fulani kikitoka.

253 Kijana, kwa kweli huko hapa kwa ajili yako mwenyewe. Uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, na huyo ni m—mtoto. Naye huyo mtoto hayupo hapa; yuko katika nchi tambarare: Kansas. Ana namna fulani ya vipindi kama kifafa. Hicho ni kifafa, kuna giza juu ya huyo mtoto.

254 Mna uhusiano fulani, au, wewe ni . . . na akina Stricker. Hivi nyinyi nyote hamkuoa dada, au kitu kama hicho? Hiyo ni kweli. Unaamini? Basi hatashikwa tena na kifafa, ikiwa utaamini kwa moyo wako wote. Kama vile umeamini, na iwe kwa huyo mtoto. Nenda sasa na usitie shaka.

Sasa unaamini kwa moyo wako wote? Nyie watu wote? Kumwombea mtu fulani. Omba na Mungu amjalie.

255 Mama huyo aliyeketi hapo, akimwombea shangazi huyo, aliye na kansa; pale chini. Unaamini kwa moyo wako wote, huko nyuma, sivyo? Sikujui wewe. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini wakati uliponisikia nikimwambia mtu huyo juu ya jambo alilokuwa akifikiria, juu ya jamaa, hilo lilikujia wewe. Sasa, unaamini kwa moyo wako wote?

256 Sasa, aligusa nini? Nataka baadhi yenu nyinyi watu, mniambie kile mwanamke huyo aligusa. Yuko futi ishirini kutoka kwangu hakuwahi kunigusa, lakini alimgusa huyo Kuhani Mkuu. Unaona, Busty? Unaona, bwana? Alimgusa Kristo. Kristo amekuja huku na kuniambia kile alikuwa akitaka, sasa amepata kile alichoomba.

Mwanamke, simjui mwanamke huyu. Yeye ni mgeni kwangu. Hiyo ni kweli? Hatufahamiani. Sijawahi kumwona maishani mwangu nijuavyo mimi, lakini Mungu anamjua. Ikiwa Mungu anaweza kuniambia jambo fulani kukuhusu kama alivyomwambia yule mwanamke kisimani, kufunua kitu kilicho moyoni mwako, utakubali, na kuamini kwamba haingeweza kuwa mimi, kama mwanadamu, ninayekwambia hilo, ingekuwa—ingekuwa ni Mungu? Ungeamini?

257 (Sasa, hawa ni wawili, au hawa ni wangapi? Tayari tumekuwa na watatu? Wawili? Wawili? Sawa. Sawa.)

258 Huyu Mwanamke ametiwa uvuli wa mauti. Kuna kivuli cheusi juu yake, ambapo ana kansa. Hiyo ni kweli. Daktari anakuambia kuwa ni kansa ya tezi ya limfu. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Umetoka mbali na hapa: Iowa. Unaamini? Una ninii, ama mtoto wa kiume, au, ni mjukuu, naye ana shida ya macho yake, nawe unamwombea. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bi. McKee, basi rudi nyumbani kwako, ukapone. Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Sikuwahi kumuona mwanamke huyo maishani mwangu. Ni kitu gani kinachosababisha hilo?

259 Ngoja kidogo. Uchaji, kidogo tu. Namtazama mwanamke mweusi moja kwa moja anayeketi hapa nyuma kabisa upande wa nyuma; nayo Nuru hiyo, mnayoiona kwenye picha ile, imening'inia juu ya mwanamke yule anayeketi kule nyuma kabisa. Niamini mimi kuwa nabii Wake, dada. Unamwombea mume wako katika hatua ya kifo kwenye Hospitali ya Kijeshi; hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini kwa moyo wako wote sasa; atapona.

Aligusa nini? Yule pale huyo mwanamke, mwanamke mweusi, mwanaume mzungu, kama yule mwanamke kisimani. Aligusa nini? Yesu yule yule. Yeye si mwanamke yule yule, yule mwanamke mweusi, au, mwanamke Msamaria alivyokuwa; yeye ni mwanamke mwingine. Mimi si Yesu, mtu yule yule; mimi ni mwanaume mwingine. Lakini yeye ni mwaminio wa Yesu Kristo, kama vile yule mwanamke alivyokuwa; nami ni mwaminio na mtumishi Wake, na Roho yule yule anafanya kazi katika siku hizi. Kristo hajafa, Yu hai. Sikuwahi kumwona wala kumjua maishani mwangu. Sasa, unaona, sio lazima uwe na kadi ya maombi upate kuwa hapa. Mwamini tu Mungu. Hiyo si ni kweli?

260 Sasa namjua mwanamke yule pale, lakini najua anachoombea: mpwa yule. Wewe amini (chini kusini), ikiwa utaamini kwa moyo wako wote, atapona.

Na wewe je? Hatufahamiani. Wewe ni kijana tu. Sijawahi kukuona maishani mwangu. Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Akiniambia, je, itakusaidia? Hakika.

Sasa, ninii tu, endeleeni tu kuamini huko nje. Mnaona?

261 Shida iko kwenye shingo yako. Ulipata ajali ya motokaa. Umekuja kutoka kaskazini. Uko karibu na Bedford, Indiana. Hiyo ni kweli. Ni kweli? Basi wewe—unaamini shingo yako itakuwa sawa? Kama unavyoamini, na iwe kwako. Rudi nyumbani umpe Mungu sifa. Pona.

U hali gani, bwana? Unaamini kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako? Unaugua ugonjwa wa—wa wasiwasi; ilikufanya ushikwe na ugonjwa wa matumbo, utumbo mpana, ugonjwa wa matumbo. Kweli umetoka California. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bw. Murray? Sawa, umekwisha sasa. Rudi nyumbani kwako; mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

Je, hatufahamiani? Sikujui wewe, na Mungu. . .Sikujui wewe na wewe hunijui. Hatufahamiani, sivyo? Ikiwa Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu, utaniamini mimi kuwa nabii Wake?

Ninyi wengine mtaamini? Mimi. . .Inanifanya niwe dhaifu sana, sana sasa, mnaona. Aminini tu sasa. Ninaninii tu. . . Upako uko hapa. Unajua hilo, sivyo? Una—unajua kuwa u—uko hapa, unaona. Roho Mtakatifu yuko hapa sasa kama unaweza tu. . .Ninazidi kudhoofika sana ni vigumu kuwaona ninyi huko nje tena. Mnaona? Wewe. . .Ikiwa kisa kimoja kilimfanya Yesu adhoofike, visa saba au vinane, kumi hapa, ambavyo tumekuwa navyo, hapa, kupitia kwenye kusanyiko hili vitafanyaje? Vitano au sita au saba hapa jukwaani pamoja na vitatu, au vinne, au vitano, huko nje. Mnaona? Imenifikisha tu mahali ambapo ni vigumu kwangu kuona tena. Inaonekana kama kwamba umati wote unakuwa kama maziwa. Laiti mngelitambua tu huo ni uzito wa Roho Mtakatifu akiingia. Hiyo ni Nuru ile, pale, inayozunguka juu ya hili jengo. Mnaona, Hiyo ni, Yeye anakuingiza kwenye mzunguko, mahali fulani.

Sasa, kwa kuwa mwanamke huyu amesimama hapa, kwenu katika mstari wa maombi sasa: Ikiwa Mungu atafunua (Hapa, nimeinua mikono yangu, sijawahi kumwona huyu mwanamke, sijui chochote juu yake.), ikiwa Mungu atafunua haswa, hebu, yale amefanya, au kile alicho, au, vema, kitu fulani kumhusu, nyinyi nyote mtaamini, basi, kwamba hiyo ni, Mungu anafanya hivyo? Mtaamini? Na je, unaweza—unaweza kukubali? Utaamini kuwa utaishi sasa? Unaweza. . .Bila shaka najua shida yako, najua shida yako, yako, haijafichwa. Unaona? Mungu hufunua mambo hayo, lakini ikiwa tu utaamini.

Sasa, nitapita na kukuwekea mikono kwa sababu ninakuwa dhaifu sana, sana. Pia najua katika muda kidogo, vema, ni—nisingeweza kuona tena, unaona.

262 Sasa, unaamini kwa moyo wako wote. Sasa kumbuka, si mimi. Mtu yeyote anajua hilo. Ni Roho Mtakatifu. Uh-huh. Sasa, laiti ningaliweza tu kuishika roho ya huyu mwanamke. Hilo ni jambo lile lile alilofanya Yesu. Kujaribu kuishika roho yake, Yeye alisema, "Nipe maji ninywe."

Huyu hapa mwanamume na mwanamke, kama tu ilivyokuwa pale. Sasa, wewe ni mwanamke mchanga, mdogo sana wa umri kuliko mimi. Sasa, labda, labda mwanamke huyu alikuwa mdogo wa umri kuliko Yesu. Alikuwa na umri wa miaka thelathini na mitatu hivi; na labda huyo mwanamke alikuwa tu na kumi na minane au ishirini, msichana mdogo tu. Na yeye—yeye—yeye karibu hakujua la kusema lakini aliposema naye Yeye alisema, "Nipe maji ninywe."

Sasa Baba alikuwa amemtuma kwenda Samaria. Alikuwa njiani kwenda Yeriko, lakini alizunguka kupitia Samaria; hiyo ni huko juu kupitia mlimani. Kwa nini alifanya hivyo? Alisema alikuwa na haja ya kupitia kule. Baba alimtuma huko. Vema, alikuja tu akaketi, na akawatuma wanafunzi mjini kununua

chakula. Basi msichana huyu mrembo akatoka kuja kuteka maji, na hapana shaka Baba alisema, “Ninamwita.”

Alisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.” Ndipo mazungumzo yakaanza. Sasa, jambo lile lile hapa.

Uliweka mkono wako kwenye koti langu? Mmoja wenu? La bwana. Mungu Mbinguni anajua Kitu kilinigusa wakati huo, wakati . . . Nilidhani ilikuwa ni Billy akiniambia niondoke. Tazama. Mimi—mimi—mikono yangu, Mungu anajua hiyo ni kweli. Kitu kilinigusa namna hiyo nami nikafikiri ilikuwa ni Billy akiniambia, “Ondoka.” Mnaona, mimi—unapokuwa hivi, ni vigumu kujua, hujui wakati wa kusimama wala jambo la kufanya. Mnaona? Karibu tu umejisahau. Nilikuwa nikiongea juu ya nini? Yule mwanamke kisimani.

Na kisha baada ya kugundua mahali ilipokuwa shida yake, basi Yeye alisema, “Nenda, kamwite mumeo.”

Akasema, “Sina yeyote.” Naye akamwambia, akasema alikuwa na watano.

Kisha akasema, “Ninaona ya kuwa Wewe ni nabii. Ninajua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya.”

Sasa huyo angeweza kuwa Masihi yeye yule leo, ikiwa ningeweza kukuambia kitu, shida yoyote? Mungu asipokusaidia, utakufa. Una kansa. Sasa, unaamini Mungu anaweza kuniambia ilipo hiyo kansa? Iko kwenye tumbo la uzazi. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Unaamini Mungu anajua unakotoka? Unatoka Illinois. Wewe ni—jina lako ni Bi. Johnson. Rudi huko upate kuishi. Yesu Kristo akuponya. Unaamini kwa moyo wako wote? Ninii tu . . . Apate kuishi . . . ? . . . Kuna sababu ya mimi kukwambia uishi.

Baba Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu sasa; upako wa Roho Mtakatifu uko hapa. Mponye, Bwana, katika Jina la Kristo, Yesu.

Mpendwa Mungu, juu ya ndugu yetu wa thamani, ambaye uliyaokoa maisha yake huko nyuma, mnamo Agosti, Ee Mungu mwenye rehema, njoo kwake sasa, wakati Roho Mtakatifu anaipaka mafuta mioyo yetu. Najua majaribu ya ndugu yangu. Mponye, Bwana, na umpe afya . . . ? . . .

Ulikuwa na mshtuko wa moyo, una ugonjwa wa kisukari; najua unaugua, hata hivyo, hiyo ni . . . ? . . .

Baba yetu wa Mbinguni, mtu huyu ni . . . ? . . . hana budi kukupata Wewe au afe. Anapenda kwenda hospitalini . . . ? . . . Msamehe dhambi zake na uuponye mwili wake katika Jina la Yesu Kristo jalia aishi. Nenda nyumbani, nenda.

Vema, hapa, ninyi nyote mpelekeni ndugu huyu nyumbani.

Mungu wetu wa thamani, katika Jina la Yesu Kristo, mikono yangu juu yake wakati upako wa Roho Mtakatifu ukiwa karibu. Jalia watu wautambue. Jalia apone.

Baba Mungu, ninapoweka mikono yangu (mikono yangu, mwili wangu haustahili, umeharibika, umeharibika na ni mvovu; lakini Roho Mtakatifu yuko juu yangu sasa), jalia nguvu zinazoweza kuyatambua mawazo ya moyo zimshughulikie mwanamke huyu na kuuponya mwili wake, katika Jina la Yesu.

Mungu mpendwa, ukimjua ndugu yangu na hali yake, ukijua ya kwamba kigugumizi hiki cha kuongea... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Ee Mungu, juu ya kijana mwanamume huyu, akipigana vita vizuri vya imani, akisimama Uweponi mwa Yehova-Yire, Dhabihu ya Bwana iliyotolewa, jalia nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini, zimguse sasa hivi. Mpe shauku ya moyo wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

263 Bwana Yesu, juu ya dada yangu ninaweka mikono yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, macho hayo na yaponywe. Jalia mateso ya—yake yaondoke mwilini mwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

264 Baba yetu wa Mbinguni, kwa ajili ya maskini Dada yangu Kidd, ninaomba kwamba utapata ushindi ndani yake, na umpe nguvu katika uzee wake kama vile ulivyompa Naomi. Bwana, naomba aendelee kutumika kwa utukufu Wako. Lijalie, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

265 Halafu kwa Ndugu Kidd, Bwana, kifo hicho kilimpata, bali Uzima ukamrudisha. Mungu, naomba kwamba utamdumisha akiwa mwenye nguvu. Ameupita kwa mbali wakati wake aliogawiwa. Lakini Wewe ni Mungu, Nawe utafanya hivi kwa utukufu Wako kama ulivyoniahidi hospitalini. Sasa, mpe nguvu kwa ajili ya ushuhuda. Ushuhuda wake usikike kupitia jimbo la Ohio, kote ulimwenguni. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Kwamba Yesu ananiponya sasa.

Nitaliamini Neno Lake...

*Mkombozi Wa Jamaa* SWA60-1002
(The Kinsman Redeemer)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 2 Oktoba, 1960, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org